




UKURASA 3

## Meneja aliyezomewa stendi ya Magufuli yamkuta makubwa


MAISHA
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili
PIKA SAMBUSA MBOGA
MITINDO
'Athleisure' mchanganyiko wa mavazi unaovutia
KATUNIKA
KARABATI NGOZI
Papai, limao, sukari inatosha

UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Mei 29, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
JUMAPILI
ISSN 0856 • No. 0580960
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# CAG KICHERE: SIOGOPI VITISHO

**AKIRI** kazi ya ukaguzi ina vikwazo vingi... *Endelea ukurasa 2*



Waandishi wa habari wa IPP Media wakiwa pamoja baada ya kutwaa tuzo za umahiri katika uandishi (EJAT) jana. Wa saba kutoka kushoto ni mshindi wa jumla wa tuzo hizo, Masekepa Masekepa. **Picha zaidi Uk. 5. PICHA: MIRAJI MSALA.**

## IPP Media yatoa mshindi wa jumla wa tuzo za EJAT

UKURASA 3

## CHADEMA yamvaa Msajili kanuni za sheria ya vyama

UKURASA 2

MICHEZO YANGA MBABE UK.24
MAONI, KATUNI UK.6




Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere (kulia), akizungumza katika mkutano na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ushirikiano wa vyombo hivyo na Ofisi ya Mkaguzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Deodatus Balile. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CAG Kichere: Siogopi vitisho

**Na Beatrice Shayo**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amesema katika kazi zake za ukaguzi tangu ashike nafasi hiyo, hajawahi kutishwa na kiongozi yeyote na haogopi vitisho.

CAG Kichere aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana wakati akijibu maswali ya wahariri wa vyombo vya habari katika mkutano ulioandaliwa na ofisi yake.

"Sijawahi kupokea vitisho, mimi siyo mtu wa kutishika, nina kanuni yangu ya kutomwogopa, kutompendelea mtu. Ukisimama katika hilo hata kama mtu ana mambo yake anataka kukufanyia, nafsi itamsuta na kuona hajaonewa.

"Ukimpendelea mtu mmoja utakuwa umemwonea mwingine, tufanye kazi kwa taratibu na kufuata kanuni zilizowekwa, utakuwa na amani," alisema.

Aliongeza kuwa yeye anafanya kazi kwa mujibu wa katiba, kufuata maelekezo yanavyomtaka na siyo kufuata maelekezo ya mtu yeyote ama taasisi.

"CAG ana uhuru wa kikatiba anapofanya kazi zake, halazimiki kufuata maelekezo ya mtu au taasisi bali nafuata taratibu," alifafanua.

CAG Kichere alisema taasisi zote zinakaguliwa na kama haipo kwenye ripoti, haina maana kwamba haijakaguliwa bali inakuwa na dosari ndogo ambazo zinatatulika.

"Hakuna taasisi isiyokaguliwa, zile ambazo hazionekani katika ripoti, katika ukaguzi wetu tumebaini changamoto zao ni za kawaida na zinatatulika kirahisi," alisema.

Aliongeza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) unakaguliwa, hata Bunge linakaguliwa, na ikionekana taasisi husika hazijatajwa kwenye ripori, maana yake dosari zake zinakuwa ndogo.

CAG Kichere alikumbusha kuwa ukaguzi walioufanya kwenye mifumo ya TEHAMA serikalini ulibaini huduma zilizopaswa kutolewa kwa wanawake ikiwamo kujifungua zimetolewa kwa wanaume.

Aliwataka viongozi wa taasisi mbalimbali za serikali na watumishi wa umma kufanya kazi kwa weledi ili kuiwezesha serikali kuwahudumia wananchi na kuwaletea maendeleo katika sekta mbalimbali.

Alikiri kwamba kazi ya ukaguzi ina vikwazo vingi kutokana na taasisi au mashirika yanayokaguliwa kuwa na kasoro nyingi zinazosababisha kupata hati chafu, hivyo kutotoa taarifa sahihi wanapofanyiwa ukaguzi.

CAG Kichere alisema ofisi yake imekuwa ikifanya ukaguzi na kutoa ripoti ya mazingira mara mbili kwa mwaka, hivi sasa wataongeza kasi ya ukaguzi kutokana na tatizo kubwa la ukataji miti linalosababisha kuharibu mazingira.

"Ofisi yangu itaongeza kasi ya ukaguzi katika sekta ya mazingira ili kuzuia uharibifu wa mazingira nchini, pia Afrika tusipoangalia tutapata shida.

"Zamani milima yetu ilikuwa inazungukwa na miti mikubwa lakini sasa hivi hakuna mti hata mmoja, kimsingi hali ni mbaya," CAG alionya.

Aliishauri serikali kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na ofisi yake ili kuboresha utawala bora, uwajibikaji kwa viongozi na kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha za serikali.

Aliishukuru serikali kwa kuwapa kibali cha kuajiri watumishi 104 akiamini kuwa ajira hizo zitasaidia kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa taasisi hiyo.

Alisema waandishi wa habari ni wadau muhimu wa ofisi hiyo na kuwataka kuandika zaidi habari za uchunguzi ili kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika vizuri kwa manufaa ya wananchi.

CAG Kichere alisema ameona nchini kuna magazeti machache ambayo yamejikita katika eneo hilo, hivyo ni muhimu kuongeza jitihada katika eneo la habari za uchunguzi.

# CHADEMA yamvaa Msajili kanuni za sheria ya vyama

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeeleza kushangazwa na hatua ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kukimbilia kuunda kanuni kwa ajili ya kusimamia mikutano ya vyama vya siasa wakati suala hilo lipo kwenye mwongozo wa Kikosi Kazi cha Rais kilichoundwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho (Zanzibar), Salum Mwalimu, alisema suala hilo lipo kwenye mwongozo wa Kikosi Kazi cha Rais kinachoshughulikia demokrasia ya vyama vingi nchini na kwamba bado hakijakubaliwa na wadau ambao ni vyama vya siasa.

Alisema wanashangaa ofisi hiyo kukimbilia kutunga kanuni hizo wakati sheria zilizoko zinajitosheleza.

Mwalimu alisema Watanzania wana matumaini na chama chao, hivyo hawatashiriki katika kuvuruga tumaini hilo.

"Hatua ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuendelea kujitafutia mamlaka zaidi katika kudhibiti shughuli za vyama vya siasa ni kupoteza muda na gharama za Watanzania bila sababu.

"Tulipokea randama kutoka Ofisi ya Msajili ikiwa na mambo 10, ikitutaka tuwasilishe maoni kuhusu kanuni za kusimamia mikutano ya vyama vya siasa lakini hatuko tayari kushiriki katika suala hili. Cha kushangaza hakuna hata moja ambalo linaonekana kuwa la maboresho," alisema.

Mwalimu alisema kwamba suala la kustaajabisha ni kwamba katika mambo yote 10 yaliyoainishwa, hakuna jipya ambalo halipo katika sheria zinazosimamia vyama vya siasa na hakuna hata moja ambalo linaonekana kuwa la maboresho," alisema.

Mwalimu alisema suala la kutunga kanuni wakati sheria hazisimamiwi inavyopasa CHADEMA inaona haliko sawa.

"Ni wazi kwamba kanuni hizi zinaundwa na waziri husika ili kutafuta namna ya kuvibana na kuvinyima uhuru wa kufanya siasa vyama vya siasa kwa manufaa binafsi," alisema.

Alidai kuwa kanuni hizo hazina nia njema, zinanuia kudhibitiana katika namna ya kuumizana hasa ikizingatiwa kuwa Sheria ya Vyama vya Siasa inaeleza wazi kuhusu haki ya kufanya mikutano ya hadhara.

Alisema katika hatua ya sasa, CHADEMA imejitokeza kukemea, kushauri na kuonya, akitoa angalizo kwamba endapo hawatasikilizwa, watajua hatua za kuchukua baadaye.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema CHADEMA inaeleza wazi msimamo wake wa tangu awali ni kutoshiriki katika suala hilo.

Moja ya majukumu ya makubwa ya kikosi kazi hicho ni kuangalia na kuchambua mwenendo wa hali ya demokrasia na namna ya kutatua dosari zinazozikumba baadhi ya vyama vya siasa, ikiwamo mikutano ya hadhara.

Kikosi kazi hicho tayari kimeshapendekeza mchakato wa kupata Katiba Mpya uanze baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Kinaundwa na wanasiasa, asasi za kiraia, wanazuoni na wadau wa kamati za ulinzi na usalama.

# IPP Media yatoa tena mshindi wa jumla EJAT

**Na Waandishi Wetu**

WAANDISHI wa habari kutoka vyombo vya habari vya IPP wameng'ara katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2021 zilizotolewa jana jijini Dar es Salaam, huku kwa mara nyingi mshindi wa jumla wa tuzo akitoka kwenye vyombo hivyo.

Katika tuzo hizo zinazotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na washirika wake, mwandishi wa Kituo cha ITV, Masekepa Masekepa, aliibuka mshindi wa jumla ikiwa ni mwendelezo kwa vyombo vya habari vya IPP kutoa mshindi wa aina hiyo.

Mwaka 2009, aliyekuwa mwandishi wa habari wa ITV na sasa Mkuu wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Jerry Muro, alitwaa tuzo ya mshindi wa jumla wa EJAT na mwaka 2018 mwandishi mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Salome Kitomari, alibeba tuzo hiyo kubwa zaidi kwenye mashindano hayo.

Mwandishi wa ITV, Jackline Silemu, aliibuka mshindi katika kipengele cha Mwandishi Bora wa Habari za Afya, huku Peter Rodgers wa kituo hicho akishika nafasi ya tatu kwenye kipengele cha Mpigapicha Bora wa Televisheni.

Kwa upande wa magazeti, Mhariri wa Habari wa Gazeti Nipashe, Sanula Athanas, kwa mara nyingine aliingia fainali ya kumsaka mshindi wa jumla wa EJAT kama ilivyokuwa katika tuzo hizo kwa mwaka 2020 zilizotolewa jijini Dar es Salaam Septemba 10, mwaka jana.

Jana Sanula aliibuka mshindi kwenye vipengele vya Mwandishi Bora wa Habari za Haki za Binadamu na Habari za Sayansi na Teknolojia.

Waandishi wengine wa Nipashe waliotwaa tuzo jana ni vipengele walivyoshinda kwenye mabano ni Sabato Kasika (Mpigapicha Bora - Magazeti) na Halfan Chusi (Haki za Binadamu). Pia wamo walioshika nafasi ya pili na ya tatu: Elizabeth Zaya (nafasi ya pili - Habari za Mafuta, Gesi na Uchimbaji Madini), Mary Geofrey (nafasi ya pili - Habari za Jinsia na Watoto) na Marco Maduhu aliyeshika nafasi ya pili (Kundi la Wazi) na ya tatu (Haki za Binadamu).

Kutoka gazeti dada la The Guardian, waandishi waliotwaa tuzo jana ni: Francis Kajubi (Takwimu), pia akishika nafasi ya pili (Uchumi, Biashara na Fedha); Beatrice Philemon (Utalii na Uhifadhi) na Muhidin Msamba (Mchora Katuni Bora). Wengine walioshika nafasi ya pili ni: Christina Mwakangale (Afya) na Jenifer Gilla (Utalii na Uhifadhi).

Katika hafla ya tuzo hizo jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitoa wito kwa wanahabari kuzingatia miiko na kanuni za kimaadili zinazoongoza taaluma hiyo na kuweka kipaumbele kwenye ustawi wa Taifa badala ya maslahi binafsi.

Alisema wanahabari wanapaswa kutambua kuwa habari ni bidhaa ya jamii na siyo bidhaa ya kuuzwa, hivyo wanawajibika kwa umma na wanapaswa kutetea maslahi ya Taifa.

"Wanahabari wenye weledi na wanaozingatia maslahi ya Taifa ni chachu ya kutimiza dhima ya kuleta mchango kwa taifa," alisema na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa waandishi wa habari na vyombo vya habari kutekeleza majukumu yao.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema serikali imesikia kilio cha MCT kuhusu uendeshaji wa tuzo hizo na itachukua jukumu la kusaidia uendeshaji wake.

■ **Imeandikwa na Mary Kadoke na Halfan Chusi**



Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Hatch, Ali Khalid (kushoto), akiwaonyesha kifaa maalum cha kusaidia kuhifadhia watoto njiti baadhi ya washiriki katika uzinduzi wa BILIx chini ya Shirika la Hatch Technologies kwa kushirikiana na mradi wa Nest 360 na Kampuni ya Anudha. Kutoka kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hatch, Dick Oranja, Mkurugenzi Mtendaji wa Anudha, Anurag Hassija na Mratibu wa Huduma za Watoto wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Dk. Felex Mundala. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Meneja aliyezomewa stendi Magufuli yamkuta makubwa

**Na Beatrice Shayo**

MENEJA wa kituo kikuu cha mabasi cha Magufuli kilichoko Mbezi mkoani Dar es Salaam, Laurent Cheche, ameondolewa katika nafasi hiyo na kurudishwa kwenye kituo chake cha kazi ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili.

Kuondolewa kwa meneja huyo kumetokana na ziara ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, wiki hii alipopokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wa kituo hicho.

Wafanyabiashara hao walimlalamikia meneja huyo, wakimtuhumu kujihusisha na vitendo vya rushwa, kutokuwa na uhusiano mzuri na wafanyabiashara hao na hana uwezo wa kukiendesha kituo hicho.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Beatrice Dominic, alipoulizwa na Nipashe jana kuhusiana na kuondolewa kwa meneja huyo alibainisha kuwa mfanyakazi huyo ameondolewa kituoni huko ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili.

"Mimi kama kiongozi wake sijamsimamisha kazi, ameondolewa kituoni ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zilizotajwa na wafanyabiashara," alisema Dominic.

Aliongeza: "Amerudishwa kwenye idara yake ya awali ya utumishi. Kama ikibainika hizo tuhuma ni za kweli, hatua zitachukuliwa, huwezi kumchunguza mtu huku akiendelea na kazi."

Mei 25, mwaka huu, meneja huyo alijikuta katika wakati mgumu baada ya kuzomewa na wafanyabiashara wakati akijibu tuhuma zake huku wakitaka aondolewe kwenye uongozi wa kituo hicho.

Baadhi ya wafanyabiashara walitoa malalamiko yao katika ziara hiyo ambapo Shaka alitaka kila kiongozi aliyetajwa atolee ufafanuzi.

Mwenyekiti wa Mawakala wa Makarani wa Mabasi mkoani Dar es Salaam, Efreim Mwambela, alisema baadhi ya wawakilishi wa serikali wapo tayari kuiangusha serikali yao.

Alidai meneja alieleza hayupo tayari kufanya kazi nao na kwamba yupo tayari kufanya kazi na matajiri.

"Kama hayupo tayari kufanya kazi na sisi, aende kufanya kazi na matajiri huko mkoani ila tunasena aondoke kwanza, hana uwezo wa kukiendesha hiki kituo," alidai.

# Chongolo ashangazwa na utendaji wa MSD

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameshangazwa na kitendo cha Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kushindwa kupeleka vifaa katika Hospitali ya Halmashauri ya Usheti, hivyo kukwamisha utoaji huduma ya matibabu.

Alionyeshwa kushangazwa huko jana akikagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo hospitali hiyo iliyoko wilayani Shinyanga, baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mbunge wa Ushetu, Immanuel Cherehani.

Cherehani alibainisha kuwa majengo ya hospitali hiyo yameshakamilika lakini utoaji wa huduma unakwamishwa kutokana na ukosefu wa vifaa tiba na uhaba wa watoa huduma.

"Wananchi wa Ushetu wanatembea kilomita 45 kwenda kutafuta matibabu.

Tulipokea Sh. milioni 300 zilizokwenda kumalizia majengo na zahanati toka mwaka 2005 na hospitali nyingi zimejengwa lakini changamoto kubwa ni vifaa tiba.

"Halmashauri yetu kupitia Baraza la Madiwani iliidhinisha Sh. milioni 48 kulipa MSD, lakini mpaka leo (jana) ni miezi sita hakuna vifaa tiba wala dawa zilizoletwa. Juzi walipata watu ajali lakini ilibidi wapelekwe Kahama mjini kwa sababu hospitali iliyoko karibu haina dawa," alisema Cherehani.

Kutokana na taarifa hiyo, Chongolo alisema serikali inajitahidi kutoa fedha na kujenga hospitali ikiwa na nia ya kusogeza huduma ya matibabu karibu na wananchi, huku akionyesha kushangaza baada ya kukagua hospitali hiyo na kukuta huduma zinatolewa pekee katika idara ya wagonjwa wa nje (OPD) tu.

"Kule huduma ya mama na mtoto haijaanza kufanya kazi na maeneo mengine. Mnasema mmelipa milioni 48 MSD lakini najua kuna mgawo wa vifaa ambavyo vimetengwa kwa ajili ya kuja kwenye hivi vituo na hospitali za wilaya.

"Nitakachofanya nitazungumza na waziri, lakini nimemwelekeza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amwite mtu wa MSD na kesho (leo) tupate majibu ya hatua za haraka wanazichukua kuhakikisha vifaa tiba vinakuja hapa haraka sana," alisema Chongolo.

Aliongeza kuwa, ndani ya mwezi huu na ujao vifaa hivyo ni lazima viwe vimefika katika hospitali hiyo ili vianze kutoa tiba na huduma kwa wananchi.

"Pesa imelipwa kila kitu kipo kuvileta tu nayo inakuwa tena mzozo na hadithi nyingine. Kwa hilo hatuko tayari. Tuliahidi kuwahudumia wananchi kupitia ilani yetu ya 2020-25 na huduma ni lazima ifike mwisho kwa kuhakikisha inaleta

## KUPAA BEI YA MAFUTA

# Macho sasa yaelekezwa matumizi ya gesi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

- DIT: Kila siku wastani wetu ni magari matano tunaweka mfumo wa gesi asilia
- Vituo vipya vya gesi kujengwa mikoani

KUTOKANA na bei za mafuta ya petroli na dizeli kuwa juu, imebainisha kuwa sasa kunashuhudiwa mwamko mkubwa wa watu kukimbilia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kuweka mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari yao ambapo kwa siku wastani wa magari manne hadi matano yanafungwa mfumo huo.

Wakati hali ikiwa hivyo DIT, katika mwaka ujao wa fedha (2022/23), serikali imesema itajielekeza kupanua wigo zaidi wa matumizi hayo ambapo itajenga vituo vya kujaza na kuuza gesi vitano kwenye mikoa mikubwa nchini, huku usambazaji wa nishati hiyo kwa matumizi ya majumbani ukianza kufanywa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC).

Akizungumza na Nipashe kwa simu jana, Mratibu wa Mradi wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari (CNG Vehicle Project) kutoka DIT, Dk. Esebi Nyari, alisema kuwa baada ya bei za mafuta kuongezeka, wateja wengi wanaulizia na kuweka mfumo huo kwenye magari yao ambapo hadi sasa magari zaidi ya 1,000 yanatumia gesi.

"Wateja wanaoulizia ni kutoka mikoa mbalimbali nje ya Dar es Salaam, lakini gesi hii inapatikana Dar es Salaam na wateja wanaonufaika ni wa Dar es Salaam. Kwa mfano, Dodoma gesi haijafika ingawa kuna jitihada za kufikisha gesi hiyo, baada ya kuongezeka wateja sisi DIT tumejipanga kuhakikisha tunawahudumia," alisema.

### MAFUNZO KWA VIJANA

Mratibu huo alisema wameanzisha mafunzo ya muda mfupi ambayo yanalenga kuwajengea uwezo vijana ili kufunga mifumo hiyo kwenye magari.

"Hadi sasa tuna vijana 32 wameshafahamu jinsi ya kufunga mfumo huu kwenye magari na hawa wapo hapa hapa Dar es Salaam, lakini tunakwenda kuendesha mafunzo mengine mwezi huu mwishoni tarehe 30, kuna kozi nyingine ya kuwajengea uwezo, nia ni kuona vijana wengi wanapata mafunzo ili kufunga mfumo huu kwenye magari," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa kuna vituo viwili vya kujazia gesi ambapo kimoja kipo Ubungo na kingine Tazara mkoani Dar es Salaam.

"Kwenye hivi vituo viwili kumeonekana wateja ni wengi na kuwalazimu kutoa huduma kwa saa 24, kwetu (DIT) ukiacha wateja wa magari ya kawaida, tulikuwa na mradi wa kiserikali, wa TPDC ambapo walileta magari zaidi ya 149, katika mradi huo tunapokea magari manne hadi matano kwa siku tunayafunga mfumo," alisema.

Akizungumzia kuhusu gharama, Dk. Nyari alisema kwa gari lenye CC 1,000 hadi 2,000 mfumo unafungwa kwa Sh. milioni mbili, kwa CC 2,000 hadi 3,000 gharama ni Sh. milioni 2.2 na zenye uwezo zaidi ya hapo ni Sh. milioni 2.8.

"Kilogramu moja ya gesi inalingana na lita 1.5 ya petroli, ukiwa unatumia gesi ukiwa na kilo moja ni mara mbili ya petroli, kwa kuwa gesi ya kilo moja inaweza kukufanya ukatembea umbali wa kilomita 20 wakati lita ya petroli utatembea kilomita 12," alisema.

Alisema kilogramu moja ya gesi inanunuliwa kwa Sh. 1,550 huku petroli lita moja ikiwa Sh. 3,170.

### VITUO MIKOANI

Wakati wa maonyesho ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati kwenye viwanja vya Bunge wiki hii, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema vituo vipya vya kujazia gesi viwili vitajengwa mkoani Dar es Salaam na vingine katika mikoa ya Dodoma na Mwanza, Arusha na Mbeya.

"Mwaka huu wa fedha tumepanga kujenga vituo vitano vya kujaza gesi ambavyo vitakuwa vikijaza kwenye magari lakini na maeneo mbalimbali halafu tutandaze zile bomba kwa ajili ya kupeleka majumbani.

"Hivi sasa ni nyumba 1,000 za mikoa ya Mtwara, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Pwani zimeunganishwa na huduma ya gesi hii," alisema.

Hata hivyo, Byabato alisema katika kupanua wigo wa matumizi ya gesi hiyo, usambazaji hautafanywa na TPDC pekee yake bali watashirikiana na REA ambao watakuwa na mpango mkubwa wa kupeleka gesi ya kupikia.

Byabato alisema watafanya kazi na sekta binafsi kwa sababu wao kama serikali hawataweza kuifanya kazi hiyo ya kupanua wigo wa matumizi ya gesi pekee yao.

Pia alisema kuna mwitikio mkubwa wa matumizi ya gesi lakini hadi sasa anayeweka mfumo huo kwenye magari ni mmoja tu, ambaye ni DIT.

# TALGWU yataja sababu kumpiga 'stop' mzabuni wa sare za Mei Mosi

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU), Rashid Mtima, amesema anasimamia haki na kutekeleza wajibu wa kama kiongozi.

Mtima aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu sababu ya kukataa kupokea sare za maadhimisho ya Mei Mosi kutokana na kukosewa.

Alisema hakuna hasara yoyote iliyosababishwa na ofisi yake, akidai kuna wafanyakazi ambao hawakuwa waaminifu aliwaondoa kazini ndiyo ambao wamejipanga kumchafua katika vyombo vya habari kuhusu suala hilo.

Mtima alisema mchakato wa ununuzi wa sare za Mei Mosi mwaka huu ulizingatia taratibu zote za ununuzi kwa mujibu wa kanuni za ununuzi za chama za mwaka 2018.

Alisema mzabuni aliyepatikana katika tenda hiyo alipewa kazi ya uchapaji na usambazaji wa sare 80,000 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.1.

Mtima alisema baada ya mapokezi ya sare ikilinganishwa na makubaliano kwa mujibu wa mkataba, ofisi ilichukua uamuzi wa kumjulisha mzabuni kuhusu upungufu huo na kumtaka kusimamisha kazi ya usambazaji.

Alisema walitoa taarifa kwa makatibu wa mikoa ambao walishapokea kutozigawa sare hizo kwa wanachama kwa sababu zilikuwa na kasoro.

Alisema mzabuni huyo alilipwa Sh. milioni 700 ikiwa ni fedha za awali na siyo kweli kwamba alilipwa Sh. bilioni 1.1 inavyodaiwa.

Alisema mchakato wa ununuzi wa gari lake ulizingatia taratibu zote za kanuni za ununuzi za chama toleo la mwaka 2018, bajeti ya chama na hali ya kifedha.

Mbali na hilo, akiongozi huyo alisema TALGWU haikuwahi kudhamiria kununua gari jipya kwa kuwa haikuwa na uwezo wa kutenga Sh. milioni 400 kwa ajili ya suala hilo.

Mtima alisema chama kilitenga fedha kwa ajili ya kununua gari la mtumba aina ya Toyota Land Cruiser V8 na walifuata taratibu zote za ununuzi kwa mujibu wa kanuni za ununuzi za chama.




Ofisa wa Mamlaka ya Mapato TRA, Chama Siriwa (kulia), akitoa elimu kwa wananchi ili kuhamasisha kutumia TRA ETS Hakiki App kwa kuipakuwa (download) kwenye simu zao, ili waweze kuhakiki vinywaji kuepukana na bidhaa feki iliyofanyika mkoani Manyara hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WASHINDI WA TUZO ZA EJAT IPP MEDIA



Mwandishi wa Habari wa ITV, Masekepa Masekepa (kushoto), akipokea tuzo ya mshindi wa jumla wa EJAT 2021, aliyokabidhiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, jijini Dar es Salaam jana.




Mhariri wa Habari Nipashe, Sanula Athanas, akipokea tuzo ya mwandishi bora wa habari za haki za binadamu aliyokabidhiwa na Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, katika hafla iliyofanyika hoteli ya Serena, jijini Dar es Salaam jana.




Mwandishi wa Habari wa gazeti la The Guardian, Beatrice Philemon, akipokea tuzo ya uandishi bora wa habari za Utalii na Uhifadhi.




Mchora katuni wa kampuni ya The Guardian Ltd, Muhidini Msamba (kushoto), akipokea tuzo ya mchoraji bora wa katuni aliyokabidhiwa na Abubakar Famau ambaye ni Mwandishi wa BBC.



Fransis Kajubi, mwandishi wa habari katika gazeti la The Guardian, akipokea tuzo ya Mwandishi Bora wa Habari za Takwimu, aliyokabidhiwa na Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe.



Mwandishi wa Habari wa Nipashe, Halfani Chusi, akipokea tuzo ya  Mwandishi Bora wa  Habari za Haki za Binadamu.



Mpigapicha Bora wa Mwaka, Sabato Kasika (kushoto), akipokea tuzo yake aliyokabidhiwa na Imane Duwe ambaye ni Mkufunzi wa Habari. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# BRELA imeonyesha njia, taasisi zingine zifuate

WAKALA wa Usajili wa Majina ya Biashara na Leseni (BRELA), juzi ulitangaza kusudio la kutaka kuzifuta kampuni za biashara 5,676 katika daftari lake kutokana na kukosa vigezo vya kisheria kuendelea kuwapo au kufanya kazi.

Hatua ya BRELA inatokana na matakwa ya kisheria ya kampuni kutakiwa kuwasilisha taarifa za mwaka kwa kampuni zilizosajiliwa nchini au mizania ya mwaka kwa kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi. Kampuni hizo ambazo zinakusudiwa kufutwa katika daftari la usajili, zimekiuka sheria hiyo kwa zaidi ya miaka 15.

Licha ya kusudio hilo, BRELA katika taarifa yake, hatua hiyo itachukuliwa kwa awamu na kwamba kati ya kampuni hizo, 5,284 zimesajiliwa nchini na zingine 392 zimesajiliwa nchi za nje na kupata hati ya utambuzi. Pia hatua ya kampuni hizo kushindwa kutimiza matakwa ya kisheria, imesababisha baadhi ya wahitaji kushindwa kutumia majina hayo ya kibiashara.

Sambamba na hilo, kwa kampuni hizo kushindwa kufanya kazi na kutowasilisha taarifa kama inavyotakiwa kisheria, kumesababisha pia serikali kukosa mapato ambayo yanatokana na kodi mbalimbali ambazo zinetokana na kazi za kampuni hizo. Kwa kufanya hivyo kumesababisha ukakasi kwenye makadirio ya kodi za biashara husika kama ilivyokadiriwa na serikali kupitia utendaji wa kampuni hizo.

Pamoja na kusudio hilo la BRELA kutaka kuzifuta kampuni hizo, imetoa muda wa kujitathmini na kufanya marekebisho ili kuepuka hatari hiyo. Kupewa muda kwa kampuni hizo kufanya marekebisho kumeonyesha kwamba serikali inazithamini na kuzihitaji ili zichangie katika maendeleo ya nchi.

Kwa hakika, hatua ya BRELA imeonyesha dhahiri kwamba serikali haipendi kufanya mambo kinyume cha sheria ikiwamo kuwa na utitiri wa kampuni za kibiashara zisizo na tija. Kwa mantiki hiyo, kampuni hizo hazina budi kuhakikisha zinatimiza matakwa ya kisheria kwa kutumia muda uliowekwa ili kukamilisha mambo yao kabla panga halijazipitia.

Pamoja na hayo, BRELA inapaswa kupongezwa kwa kazi hiyo kwa sababu kumekuwa na kampuni nyingi za mifukoni ambazo baadhi zimekuwa zikipewa kazi bila kuwa na usajili au kutokuwa na vigezo. Hatua hii ya BRELA itaziamsha kampuni na taasisi ambazo zimekuwa zikitoa kazi kwa baadhi ya kampuni bila kujua kama zina usajili au zimetikiza matakwa ya kisheria kama kuwasilisha taarifa za kodi na hesabu za kila mwaka.


Kama itakumbukwa, Tanzania iliwahi kuingia mkataba na kampuni moja ambayo usajili wake ulikuwa na utata na kupewa kazi ya kufua umeme na matokeo yake nchi ikaingia katika kashfa kutokana na kutokuzalishwa hata kwa megawati moja ya umeme.

Kadhalika, BRELA imeionyesha mfano kwa taasisi zingine za serikali kuchunguza na kufuatilia kampuni mbalimbali ambazo zimesajiliwa kwenye vyombo hivyo husika ili kuhakikisha zina usajili halali kwa mujibu wa sheria badala ya kuendesha mambo yao kwa ujanja ujanja.

Miongoni mwa taasisi hizo ni zile zilizopewa dhamana ya kusajili wataalamu na watu kama makandarasi, wahandishi, wakadiriaji majenzi, wathamini wa ardhi, wahasibu na wakaguzi na wataalamu wa ugavi na ununuzi.

Kwa kufanya hivyo, ni dhahiri kwamba nchi itakuwa na watu au kampuni zinazofanya kazi kwa weledi badala ya kuwa na vishoka ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa viwango vya chini na matokeo yake kusababisha miradi mingi kufanywa katika viwango duni na serikali kupata hasara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ushauri wa Profesa Mkumbo unaweza kusaidia kuinua elimu

Na Sabato Kasika

**KAULIMBIU** ya maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani mwaka jana, ilikuwa "Walimu katika kiini cha kupona kwa elimu," ikilenga kuonyesha jinsi ambavyo wana mchango mkubwa kwenye sekta hiyo.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa wanakabiliwa na vikwazo vingi ambavyo vinachangia kuwafanya wasitekeze majukumu yao ipasavyo na wamekuwa wakiomba wawezeshwe kwa kila hali ili waifanye kwa ufanisi. Mojawapo wa uwezeshwaji huo ambao wamekuwa wakiutamani ni mafunzo, ukuzaji wa taaluma, msaada na mazingira ya kazi wanayohitaji kupeleka vipaji au talanta zao, lakini pia uboreshaji wa maslahi yao.

Hatua hiyo hiyo na nyingine, zinaweza kusaidia ufufuaji wa elimu ikiwa zitatekelezwa kikamilifu na sauti na nafasi ya kushiriki katika kufanya uamuzi kwa mambo yanayohusu maslahi yao.

Vikwazo hivyo vya walimu vinamwibua Mbunge wa Ubungo Dar es Salaam, Profesa Kitila Mkumbo, ambaye anakuja na ushauri ambao kwangu ninaona unaweza kusaidia kuinua elimu nchini iwapo utazingatiwa.

Akichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu ya mwaka 2022/2023 bungeni jijini Dodoma hivi karibuni, anaishauri serikali kurudisha utaratibu wa kutoa kwa walimu ili kuwaongezea motisha ya kufanya kazi.

Katika ufafanuzi wake, anasema walimu wanatakiwa kupewa posho ya Sh. 4,000 kwa siku, na kwamba kwa mwezi mmoja anapaswa kulipwa Sh. 100,000 kiasi ambacho anabainisha kuwa serikali haiwezi kushindwa kutoa.

Msomi huyo pia anagusia suala la kufuta kada ya maofisa elimu kata ili kuziba pengo la walimu katika shule mbalimbali nchini, kwamba ni muhimu kupunguza utawala katika elimu ili kuimarisha menejimenti ya shule.

Prof. Mkumbo anatamani kuona maofisa elimu kata hao wakienda shuleni kufundisha huku serikali ikiajili walimu 20,000 hadi 30,000 kwa mwaka ili kuziba pengo la walimu wanaohitajika.

Katika ushauri wake huo, anatamani muda wa mafunzo ya ualimu uongezwe kutoka miaka mitatu hadi miaka minne ili wanapohitimu, wawe wameiva kwa ajili ya kufundisha kwa vitendo. Ushauri huo unegefaa kuchukuliwa kwa uzito unaotakiwa, hasa kwa kuzingatia kwamba walimu ni wahusika wakuu wa juhudi za kufufua elimu na ni wa muhimu katika kuharakisha maendeleo kuelekea elimu bora iliyo jumuishi na yenye usawa kwa kila mwanafunzi, katika kila hali.

Wao ndio wanaoibua viongozi wa baadaye, madaktari na wataalam wa fani mbalimbali, hivyo ninadhani suala la kuwawezesha kwa kila hali ili wafanye kazi yao kwa moyo mkunjifu ni la kupewa kipaumbele.

Lakini pia walimu pia wamekuwa kiini cha kielimu, kuanzia katika kutumia teknolojia kwa ubunifu hadi kutoa msaada wa kijamii na kihisia kwa wanafunzi wao ili waweze kufikia malengo waliojiwekea kwenye elimu.

Hivyo kama itakuwa vigumu kuwawezesha kwa kila kitu, lakini japo suala la hiyo motisha ya Sh. 4,000 kwa siku lingesaidia angalau kuwafanya waendelee kuwa na moyo kujituma hata kwenye mazingira magumu.

Ikumbukwe kuwa zipo baadhi ya shule zina walimu wachache, huku idadi ya wanafunzi ikiwa kubwa, ninaamini kwamba katika mazingira hayo, utendaji kazi wao hauwezi kuwa na ufanisi. Hivyo, jambo la muhimu ambalo lingesaidia kuwafanya wakabiliane mazingira hayo wakati serikali ikiendelea kuajiri walimu wengine, ninaona ni kuwapa motisha ya posho ya Sh. 4,000 kama aanavyoshauri Prof. Mkumbo.

Kuwapo kwa posho hiyo kunaweza kusaidia kumaliza msuguano kati ya wazazi na walimu ambao wamekuwa wakituhumu baadhi ya walimu kuwa wanalazimisha wanafunzi kufanya 'twisheni' ili wapate fedha.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tuna uwezo kutengeneza Watanzania matajiri iwapo tutafanya mambo haya



Na Pascal Mayalla

NAENDELEA na makala zangu za kuelimishi kwa maslahi ya taifa kwa kuuliza maswali ambayo yakipatiwa majibu mujarabu, yatalibadilii taifa kutoka hapa tulipo na kupiga hatua mbele zaidi kimaendeleo.

Kunapotokea tatizo mahali, ili kulitatua, hatua ya kwanza ni kulitambua tatizo, yaani kukijua chanzo cha tatizo baadaye kutafuta ufumbuzi mwisho kuchukua hatua za kulifumbua.

Tukubali, tukatae, mfumo wetu wa elimu una matatizo. Tunafundishwa elimu ya nadharia kwa kutumia modali za wenzetu ambao hatufundishiwi kutatua changamoto zetu bali ni elimu ya nadharia kubwa, lakini vitendo vichache.

Mfano, Tanzania tuna elimu ya fasihi (literature) hadi chuo kikuu, tuna maprofesa na wasomi nguli wenye shahada za uzamivu (Ph.D) za fasihi makumi kwa mamia kutoka tangu miaka ya 1960, vyuo vikuu vyetu, toka miaka ya 60. Binafsi nimesoma fasihi sekondari hadi chuo kikuu, lakini hakuna hata kitabu kimoja cha fasihi kilichoandikwa na maprofesa wetu ambacho kilitumika kufundishia. Vitabu vyote ni vya waandishi kutoka nchi za wenzetu!

Vitabu vya karibu ni vya majirani zetu, Ngungi wa Thiongo, "The River Between" na Okot T'Bitek "Song of Lawino". Lakini tumefundishwa literature za Chinua Achebe "Things Fall Apart" na kina Henrik Ibsen "An Enemy of The People". Wote hawa ni waandishi wa nje. Jambo la kujiuliza hivi wasomi wetu wa fasihi wa vyuo vikuu wako wapi? Jibu ni wasomi wa nadhariia tu.

Nikiwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), nilikuwa natembelea maktaba kuu ya chuo. Ukiwa ni mwandishi wa habari, mwenye damu ya habari za uchunguzi, ukifika mahali popote lazima tu utachunguza hata kwa kupepesa macho.

Sasa ukifika maktaba ya Chuo Kikuu, sehemu za tasnifu za Ph.D utakuta ziko kwa mamia zenye utafiti na majawabu ya matatizo yetu kwenye makabrasha yakila vumbi tu.

Ni taarifa za utafiti ambazo hazifanyiwi kazi. Kwa kuwa lengo la tasnifu hizo ni kwa ajili ya kupata shahada, watafiti hao wakishatunukiwa Ph.D zao, kazi ndiyo imeishia hapo kwa hiyo kilichotafitiwa kinaishia kwenye makabrasha.

Ukifanyika utafiti wa mamilionea na mabilionea 100 Tanzania, utashangaa kukuta nusu waliishia darasa la saba na unaweza kukuta hakuna milioneo au bilionea yeyote ambaye ni mhitimu wa chuo kikuu chetu. Hii ni kwa sababu tunafundisha elimu ya nadharia na si elimu ya vitendo kuwezesha watu kujitegemea.

Bilionea mdogo kabisa kwa sasa ni Diamond Platinum, yeye aliishia darasa la nne! Bilionea wa ukweli namba moja Tanzania mwenye 'impact' kubwa kwa maisha ya wengi, naomba nisimtaje jina, ila hakusoma hata darasa moja zaidi ya elimu ya madrasa.

Hii maana yake, Tanzania hatuwezi kupata maendeleo ya kweli kwa kuwategemea wasomi wa elimu ya kizungu ya darasani. Tutapata maendeleo ya kweli kwa kuwajengea uwezo, Watanzania wenye vipaji vya biashara kwa kuwapatia mitaji.

Mwasisi wa Tanganyika na baadaye Taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere kwa kilijua hilo, alianzisha elimu ya kujitegemea ili mwanafunzi akimaliza darasa la saba apate upeo wa maisha na kujitegemea. Nyerere alipomaliza kipindi chake, aliondoka na siasa yake ya Ujamaa na Kujitegemea, Siasa ni Kilimo, Uhuru ni Kazi na Elimu ya Kujitegemea.

Enzi za ukoloni, watu walioishi maeneo ya Oysterbay walikuwa wazungu. Baada ya kupata uhuru, maeneo hayo waliishi maofisa wa juu wa serikali. Enzi hizo za Mwalimu Nyerere na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, maofisa wa serikali walioishi Osterbay, walirejea vijijini kwao na kuendelea kuishi kwenye majumba poromoka!

Enzi ya Mkapa, ikaamuliwa maeneo hayo wauziwe viongozi wa serikali na baada ya kuuziwa ukipita Oysterbay na Masaki za leo, utaona mijengo ya maana. Zile nyumba zilizokuwa Oysterbay ya zamani, nyingi zimebomolewa na kujengwa mijengo ya kisasa. Lakini ukifanywa utafiti kuangalia ni Watanzania wangapi wanaishi Osterbay na Masaki, unaweza usiamini. Idadi ya wageni ni kubwa zaidi kuliko wazawa kwa sababu wengi hawana uwezo wa kuishi maeneo hayo.

Kinachofanywa na wawekezaji ni kuwanunua wazawa, kupisha na kuwekwa uwekezaji wa maana, lakini laiti wazawa wamiliki wa maeneo hayo wangejengewa uwezo wa kimitaji, wawekezaji wakaingia ubia na wazawa hao, sasa hizi tungejikuta Osterbay na Masaki zote zinamilikiwa na mazawa na wote ni mabilionea.

Kazi ya kutengeneza mabilionea wa Kitanzania, ndicho kitu kinachofanywa na kampuni ya mafuta ya TotalEnergies, kupitia mpanga wake uitwao DODO. Kupitia mpango huo, Watanzania wenye maeneo ya pembezoni mwa barabara kuu, wanajengewa uwezo wa kumiliki kituo cha mafuta na kufundishwa uendeshaji wa biashara.

Chini ya mpango huo, TotalEnergies, imeendelea kumwaga fursa kwa Watanzania kumiliki vituo vya mafuta. Katika mwendelezo wa kutimiza azma hiyo, wiki hii kampuni hiyo ilizindua kituo cha mafuta cha 14 kinachomilikiwa na Mtanzania eneo la Mapinga, Bagamoyo mkoani Pwani na kuwaomba Watanzania wengine wenye maeneo kando ya barabara kuu, kuchangamkia fursa hizo kujengewa vituo vya mafuta vyenye jina la kampuni hiyo na kuviendesha kwa ubia.

Mkurugenzi Mkuu wa TotalEnergies Tanzania, Jean-Francois Schoepp wakati wa ufunguzi wa kituo hicho, alisema DODO ni fursa nzuri kwa Watanzania wenye maeneo ya kando ya barabara, kuingia kwenye biashara ya mafuta na kampuni itawapatia kila usaidizi ili Watanzania wengi zaidi wamiliki vituo vya mafuta.

Mmiliki wa kituo hicho, Jackson Swai, na mkewe Joyce, waliishukuru TotalEnergies kwa kuwafungulia fursa hiyo na kuishukuru Benki ya NMB kwa kuwapa mkopo wa ujenzi wa kituo hicho.

Kwa mfumo huo, Watanzania wakiwezeshwa kwa mbinu za kisasa za biashara na kupewa mitaji, kuna uwezekano mkubwa wa kutengeneza mamilionea na mabilionea wengi ambao watachangia uchumi na pato la taifa pamoja na kuibua ajira kwa vijana wetu.

**Wasalaam.**
**Paskali**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hakika tunafanya vibaya kubana wabunifu



Na Joseph Kulangwa

**Wawili hawa wakaja kuwa maarufu sana kijijini na vijiji jirani ambavyo viliwatumia katika kupata silaha, lakini pia umaarufu wa mcheza sarakasi nao ukawainua kwa kutangazwa kijiji cha mcheza sarakasi, hivyo vijiji vya jirani na waridi navyo vikanukia.**

NAKUMBUKA zamani tukiishi kijijini, tulikuwa na babu mnoko sana ambaye hakupenda kuona wajukuu wakorofi. Kwa bahati mbaya alikuwa na wajukuu lukuki, hivyo kichwa kilimzunguka kila kulipokucha.

Ni kweli wajukuu zake walikuwa watundu sana. Mmoja alikuwa anapendelea kuchongachonga vitu na mara nyingi silaha kama mishale na pinde, lakini vikiishia kuumiza wenzake.

Mwingine alikuwa kama ngedere, akiparamia miti kila wakati na wakati mwingi hakukosa majeraha tena mengi ya kuvunjika viungo kutokana na kuporomoka na matawi ya miti.

Babu aliwakemea sana, lakini haikufua dafu na hatimaye akachoka na kuwaacha hata alipotangulia mbele za haki. Wajukuu walilia na kusahau na kuendelea na utundu wao na safari hii kwa uhuru zaidi.

Kumbe hatukujua kuwa walikuwa na vipaji fulani vya kufanya mambo, huyu mchonga mishale kumbe akaja kuwa fundi mzuri tu wa silaha hizo za jadi na kuanza kuziuza na kujipatia kipato. Huyu mwingine akawa mcheza sarakasi mzuri akifanya maonyesho yake sehemu mbalimbali na kujiingizia kipato kizuri kilichomsaidia yeye, wadogo zake na familia kwa ujumla, hivyo wa karibu naye wakajivunia.

Wawili hawa wakaja kuwa maarufu sana kijijini na vijiji jirani ambavyo viliwatumia katika kupata silaha, lakini pia umaarufu wa mcheza sarakasi nao ukawainua kwa kutangazwa kijiji cha mcheza sarakasi, hivyo vijiji vya jirani na waridi navyo vikanukia.

Ni kweli kwamba utundu wao ulikuwa hatari kwao na kwa wengine, lakini hata hivyo, baadaye utundu ule ukawa ubunifu na kuisaidia jamii. Ingekuwa leo, ina maana wangesaidiwa na kujipatia maarifa na kutengeneza silaha zaidi na za kisasa, lakini kupata vifaa vya sarakasi.

Hivyo ndivyo maisha yalivyo katika jamii kwamba mtu anaweza kuwa na kipaji au ubunifu fulani lakini machoni mwa wengi akaonekana wa hatari. Akishikiliwa vizuri anaweza kuonekana wa maana katika jamii na kuisaidia.

Juzi nikasikia taarifa kutoka wilaya fulani nchini, eti kuna daktari feki kakamatwa akihudumia wagonjwa tena katika jengo ambalo halijakamilika ujenzi, lakini akiwa na dawa ambazo pia zimemaliza muda wa kutumika.

Mkuu wa Wilaya katika kutelekeza majukumu yake, akaamuru polisi wamkamate daktari huyo, ili akahojiwe na kujua sababu za kufanya hivyo, wakati hana cheti wala kibali cha kumwezesha kufanya hayo. Nikasikia kuwa katika 'zahanati' yake hiyo, kuna watu walipoteza maisha.

Kwingine pia nikasikia jamaa kakamatwa akitengeneza bunduki za kienyeji. Naye huyu Dola ikamkamata, ili akaeleze ni kwa nini anatengeneza silaha bila kuwa na idhini au kibali cha serikali na kuhatarisha maisha ya watu. Wawili hawa ni mfano tu wa watu wanaojiamulia kufanya mambo yao kwa faida yao, lakini bila kujua pia kuwa ni kwa faida ya wengine. Lakini hilo halizuii kukamatwa na kuhojiwa na hata vyombo vya sheria kuwaadhibu kwa kukiuka taratibu.

Lakini twende mbele turudi nyuma, kuna mahali hakuna zahanati, hakuna kituo cha afya, hakuna chochote cha tiba ya kisasa kwa wananchi, anajitokeza mtu aliyesoma udaktari au uuguzi na ana mwanga wa kusaidia, anasaidia na watu wanapona lakini hana kibali.

Kama ni kufa hata hospitali za rufani kuna watu wanakufa tena kwa wingi tu. Lakini huyu angalau kasaidia watu fulani kwa tiba na ndiyo sababu hata walipokwenda kushuhudia 'zahanati' hiyo, wakakuta umati wa wagonjwa. Hiyo ilidhihirisha kuwa kuna watu wanamwamini, kwamba kuna wagonjwa walikwenda pale wakatibwa na kupona na kama ni kufa ni kudra za Mwenyezi Mungu, hivyo yawezekana pamoja na kwamba alikuwa akitoza malipo, lakini alifanya kwa nia njema.

Haya huyu mwingine kaweza kubuni na kutengenza silaha, na hata siku moja hatukusikia silaha alizotengeneza zimeua au kujeruhi mtu au mnyama wa mtu fulani, bali anafanya ubunifu na kama inawezekana hata kutumia bunduki kujihami na wanyama hatari au waharibifu.

Lakini wote hawa wanajikuta mikononi mwa dola kwa kukosa vibali na vyeti vya kitaaluma. Je, kama wangechukuliwa na kusaidiwa kwa mafunzo na vifaa wasingeweza kuisaidia jamii kweli, badala ya kuwakamata na kuwafunga kwa kukiuka sheria?

Sawa sheria zipo na ziheshimiwe, lakini ni vema kuangalia na mantiki yake ya kuzitumia, ni vema busara ikatangulia. Ndiyo sababu mchonga mishale akaisaidia jamii yake, lakini hata mparamia miti kwa srakasi zake akaisaidia jamii. Ni kuwaendeleza badala ya kuwafunga. Tukuze na kulea vipaji basi! **Alamsiki!**

# KWA NINI NDOA NYINGI ZA SASA ZINAVUNJIKA?

Na Dk. Enock Mlyuka

NDOA ni wajibu na ni hitaji la jamii. Ndoa ni taasisi ambayo ni kitovu cha familia na malezi. Kwa mantiki hiyo, ndoa zikiwa imara, kutakuwa na familia, jamii na taifa imara. Lakini ndoa isipokuwa imara, familia haiwezi kuwa imara wala jamii na taifa.

Ndoto na matumaini ya kila mmoja wakati anapofunga ndoa ni kufanikiwa na kuishi maisha yaliyojaa upendo, furaha na amani. Hata hivyo, mambo yamekuwa kinyume cha matarajio kwa kuwa wanandoa wengi wameshindwa kuishi maisha halisi ya ndoa.

Maisha ya baadhi ya wanandoa ni kama jangwa, muda wote hufukuta joto na kutimua vumbi. Ndoa kwa baadhi ya wanandoa imegeuka kuwa shubiri. Usanii unazidi kuongezeka na baadhi ya wanandoa wamepoteza hisia chanya na mvuto dhidi yao. Wengi wamekuwa wanaharakati zaidi katika ndoa kuliko kuwa walezi wa ndoa zao. Hali hii imesababisha migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi na kusababisha kuvurugika kwa ustawi wa familia.

Takwimu za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), taarifa za viongozi mbalimbali wa dini, jamii, mahakama na wanasheria zinaonyesha ongezeko kubwa la migogoro ya ndoa na kuvunjika kwa ndoa nchini.

Kutokana na hali hiyo, Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma katika hotuba aliyoitoa Oktoba 6, 2021 mkoani Dodoma, pamoja na mambo mengine, alibainisha ongezeko kubwa la mashauri ya ndoa na mirathi katika mahakama.

Kwa uchache, alisema kwa kipindi kati ya mwaka 2017 na 2019, mahakama za mkoa wa Dar es Salaam pekee, zilikuwa na mashauri ya ndoa takribani 4,200 na mashauri ya mirathi 7,600. Kadhalika, takwimu kutoka RITA zinaonyesha kwa kipindi cha mwaka 2020/21, zaidi ya talaka 500 zilisajiliwa kwa nchi nzima.

Baadhi ya ndoa zimedumu muda mfupi chini ya mwaka mmoja. Inawezekana talaka ni nyingi kuliko takwimu hizi kwa kuwa watu wengi hawajui kusajili matamko ya talaka kutoka mahakamani ili wapate vyeti. Pia wako wanandoa ambao hutengana na hupeana talaka mitaani kienyeji pasipo kufuata taratibu za kisheria. Hali hii ni janga la taifa ambapo hatua za makusudi zinahitajika kuchukuliwa ili kuzinusuru familia na uharibifu hasa wanawake na watoto ambao ndio wahanga wakuu.



Ndoa kama hii inapaswa kujengwa kwa msingi imara ili idumu na kustawi. **PICHA: MAKTABA.**

### ■ CHANZO CHA MIGOGORO

Hatua za kuchukua ni lazima ziende sambamba na kufahamu chanzo cha migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi za sasa. Uzoefu wangu katika huduma ya ushauri na semina ninazofanya mara kwa mara kuhusu masuala ya ndoa na familia kwa zaidi ya miaka 25, unaonyesha kuwa ziko sababu kuu sita ambazo ni chanzo cha migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Sababu hizo ni kama zifuatazo;

### ■ KUKOSA KUSUDI NA MALENGO

Watu wanaoa na kuolewa kwa malengo tofauti. Tofauti ya malengo imeleta shida kwa wanandoa wengi. Wako baadhi ya watu ambao wameoa na kuolewa kwa lengo la kutafuta ufahari na heshima katika jamii, kupata mali, fedha, vitu fulani, kulelewa, kuvutiwa na kazi anayofanya mtu kwa mtazamo kuwa kwa kuoa au kuolewa naye maisha yatakuwa mazuri na mserereko.

Halikadhalika, baadhi ya wasichana wameamua kuolewa kama njia ya kuepuka ugumu wa maisha ya nyumbani kwao. Kwa mantiki hiyo, mambo yanapokuwa kinyume na mtazamo na matarajio ndipo matatizo yanapoanza kwani mtu alichotazamia kukipata hakipati. Hapo uvumilivu unakosekana kabisa.

### ■ KUKOSA UMAKINI KATIKA UAMUZI

Watu wengi wameoana wakiwa hawafahamiani vizuri kabla katika mambo ya msingi kama vile familia wanazotoka, mila na desturi, itikadi za kiimani, haiba, tabia na mienendo. Watu wengi wamejikuta katika matatizo makubwa kutokana na uamuzi mbaya waliofanya awali. Waingereza wanasema, "Choices you make in life make you".

Mtu hawezi kuwa tofauti na uamuzi aliofanya kwani mtu siku zote huvuna alichokipanda. Vijana wengi wa sasa wametanguliza mapenzi kuliko upendo. Akipata alichokihitaji basi uhusiano unaishia hapo. Wengi wamejikuta katika matatizo kwa sababu ya kukurupuka na kuongozwa na mihemko katika kufanya uamuzi wa kutaka kuoa na kuolewa. Mtu anajikuta anaoa au kuolewa na mtu asiye na sifa za kuwa mke au mume. Si kila mwanamke au mwanamume aliyepo duniani ana sifa za kuwa mke au mume wa mtu.

### ■ KUKOSA UFAHAMU NA MAARIFA

Ndoa ni taasisi nyeti yenye misingi, kanuni, sera, taratibu na miiko yake. Watu wengi wameoa au kuolewa pasipo ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi hii. Vijana wengi wa leo hawafunzwi kabisa, hata wale wanaofunzwa, hawafunzwi vya kutosha na kuandaliwa mapema kuwa waume na wake za watu. Nguvu kubwa huelekezwa katika kuandaa sherehe za harusi na siyo kuwaandaa vijana kuwa waume na wake bora .

Kadhalika, vijana wengine hawaoni umuhimu wa kujifunza kwa sababu ya ujuaji mwingi na kujiona wanajua kila kitu kuliko hata wazazi au walezi wao, hivyo, hawashauriki. Matokeo yake wanakuwa vivuruge katika ndoa zao kwa sababu ya kutokutambua nafasi, wajibu, haki na mipaka yao katika ndoa na maisha ya kila siku.

### ■ MALEZI NA MAKUZI

Wanasaikolojia wanabainisha kwamba, zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo ni matokeo ya malezi na makuzi wakati wa utoto. Wako watu wazima leo ambao katika kukua kwao hawajawahi kuona matendo ya upendo na baraka ya baba na mama zao. Walichokishuhudia katika makuzi yao kutoka kwa wazazi wao ni matendo ya ukatili, unyanyasaji na ugomvi.

Watu wengine ni wavivu wa asili, hawawajibiki katika ndoa na maeneo yao ya kazi, waongo, wabishi, wajeuri, wanafiki, wachoyo, hawajui kupika na maarifa ya nyumbani, hawajali, watu wa kuoa na kuacha au kuachika kwa sababu wametengenezwa kuwa hivyo katika familia wanazotoka.

Kwa hiyo, wanapoishi na watu wengine wanaendeleza yale waliyojifunza kutoka kwa baba na mama au familia zao wakiamini kuwa ndio mfumo sahihi wa maisha. Hii ndio maana ya msemo wa wahenga usemao kwamba, "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo".

### ■KUKOSA HOFU YA MUNGU:

Waumini wengi ni waumini wa kimapokeo na si wa kiroho, hivyo, wengi wao wanaishi wameoa au kuolewa lakini hawajampa Mungu nafasi ya kutosha ya kuongoza maisha yao. Wengi wametanguliza zaidi elimu zao, uwezo wao wa kifedha, nafasi zao katika jamii na matamanio yao kuliko Mungu.

### ■MATATIZO AFYA YA AKILI

Wako watu ambao wamezaliwa wakiwa na matatizo ya afya ya akili, ambapo wazazi wao hawajui na wao wenyewe hawajitambui. Watu wengine matatizo ya afya ya akili wameyapata ukubwani kwa sababu ya kuvurugwa na mambo mengi yaliyojeruhi nafsi katika maisha yao na kuwa katika msongo wa mawazo kwa muda mrefu.

Utawafahamu watu wa namna hii kwa lugha zao kali na mbaya za mara kwa mara dhidi ya mtu au watu wengine, vitisho vya kuua au kujiua, matendo ya ukatili na unyanyasaji wanayoyafanya katika ndoa au uhusiano na maisha ya kila siku.

Kwa namna hii, wako baadhi ya wanandoa ambao wameoa au kuolewa na watu wenye matatizo ya afya ya akili. Hali hii imesababisha kukosekana kwa utu na kupelekea wakati mwingine baadhi ya wanandoa kujeruhiana vibaya na kufanya uamuzi mbaya wa kuondoana uhai, mahali pengine na watoto wasio na hatia.

### ■ NINI KIFANYIKE?

Jambo la msingi, vijana wasikurupuke bali wawe na malengo na kusudi jema la kutaka kuoa au kuolewa. Kijana aoe au kuolewa na mtu ambaye anamfahamu vizuri, mtu ambaye atamfurahia, atashirikiana naye katika raha na shida, shida yako ni shida yake; mtu ambaye anajali, anayejitambua, mcha Mungu, mwenye utu, anayejiheshimu, ambaye watasaidiana (kwa kutaja machache) katika kufanikisha maisha yao ya pamoja kwa umoja.

Ifahamike kuwa kutaka kuoa au kuolewa na mtu kwa msingi wa vitu au hali ni kujidanganya na kujitengenezea maumivu ya kujitakia yatakayoathiri mwenendo mzima wa maisha ya mtu. Watu wafahamu kuwa maisha ni safari ambayo ndani yake kuna kupanda na kushuka, kuumia na kufurahi, kupata na kukosa au kupungukiwa.

Watu wawe na dhamira ya dhati na jitihada ya kujifunza ili kuifahamu taasisi ya ndoa vizuri na madai yake kabla ya kuingia katika ndoa. Kutoifahamu taasisi hii ni kuchagua maumivu na kushindwa maisha ya ndoa. Vijana wa kike na kiume wanahitaji kuandaliwa mapema kuanzia ngazi ya familia ili wawe wake na waume bora. Halikadhalika, taasisi za dini ziwe na programu za muda mrefu na endelevu kuhusu ndoa, familia na malezi zenye kugusa mahitaji halisi ya jamii.

Ndoa ni taasisi nyeti ya heshima na takatifu. Si taasisi ya kuichezea na kufanya majaribio. Vijana wapate muda wa kufahamiana vizuri katika mambo ya msingi kabla ya kufanya maamuzi ya kutaka kuoa au kuolewa. Ni muhimu kufahamu familia mtu anayotoka, mila na desturi zao, itikadi za kiimani,haiba, tabia na mwenendo wake kwa kuwa mwonekano wa nje wa mtu haimaanishi kuwa ndio ubora wake.

Uamuzi wa siku moja au muda mfupi unaweza kujenga au kubomoa maisha ya mtu. Umakini unahitajika sana kwa yule unaye tamani kuhusiana naye na kumruhusu aingie katika maisha yako. Katika kuoa, mtu anapaswa kumshirikisha Mungu na kutumia uwezo wake aliokupatia wa kujua mema na mabaya (intellect) katika kufanya uamuzi sahihi kwa mtu sahihi na kwa wakati sahihi kwani kila jambo lina wakati wake.

Watu wajenge utamaduni wa kupima afya zao kabla ya kuoana ikiwa ni pamoja na kupima afya ya akili ili kuepuka matatizo yasiyo ya lazima.

Wazazi wawe mfano mwema wa kauli na matendo kwa watoto wao ili kujenga kizazi cha watu wema, waadilifu na wanaowajibika. Hata hivyo, pale mzazi anapokosea katika malezi, kijana afahamu kuwa bado anayo nafasi ya kubadili historia mbaya ya maisha yake na kizazi chake kitakachofuata. Jambo la msingi ni kujitambua, kukubali udhaifu, kudhamiria kubadilika, kujifunza, na kumruhusu Mungu kuwa kiongozi wa maisha yako.

Vikao, elimu, fedha, na nafasi tulizo nazo katika jamii haviwezi kuleta suluhu ya kudumu ya matatizo yetu yote. Kuna mambo katika maisha yetu ufumbuzi wake unamhitaji sana Mungu aingilie kati kwani uwezo wetu wa kibinadamu una mipaka na ukomo. Pamoja na jitihada zetu za kibinadamu ni muhimu watu wajifunze kumtumaini Mungu katika maisha yao.

**■Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

MEI 29, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

## PIKA SAMBUSA MBOGA





Ukurasa 13

## MITINDO

'Athleisure' mchanganyiko wa mavazi unaovutia




## KATUNIKA

Ukurasa 16





# KARABATI NGOZI

## Papai, limao, sukari inatosha

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | T | A | M | K | O |
| ■ | A | ■ | ■ | A | ■ |
| U | M | A | ■ | N | ■ |
| ■ | B | ■ | U | D | A |
| ■ | U | ■ | ■ | I | ■ |
| S | A | N | D | A | ■ |

## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
AMA, IPO, WINDA, PWANI, NYUMBA, PEPONI

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO John alikuwa alikuwa na mama yake sebuleni akifundishwa somo la historia. Mama yake alimwambia hata historia ya baba yake ilianzia mkoa wa Tabora alipozaliwa katika kabila la Mnyamwezi.

Baada ya kusikia hivyo, John alimwambia mama yake kuwa mwalimu wake alimfundisha jambo Fulani.

Mama: Mwalimu alikufundisha nini ukiwa huko shuleni?

John: Mwalimu alituambia kuwa mzigo mzito mpe Mnyawezi, na wewe umeniambia baba kabila lake Mnyamwezi, naamini ana nguvu ya kubeba vitu vizito.

Mama: Hapana huo ni mzemo tu unaomaanisha kwamba kuna baadhi ya watu wanabeba maumivu ya wengine bila kulalamika.

John: sawa mama nimefahamu

SWALI

Daraja la Mkapa ilinapatikana wapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Tambua mapema karama ndani yako ili ufanikiwe

KARIBU tena msomaji tuendelee kuchambua sababu zinazofanya watu wengi kukata tamaa katika safari ya kufikia mafanikio yao. Tayari tumeshajadili sababu tatu ambazo ni kutarajia mafanikio ya haraka, kutarajia matokeo makubwa kuliko ulivyowekeza na kutojipanga kwa yasiyotarajiwa.

Leo tujadili kutokutambua maono na karama zako mapema. Niendelee kusisitiza kwamba Mungu ameweka maono, karama na vipawa ndani yako ili ufanikiwe katika maisha. Haukuzaliwa kwa bahati mbaya, kwani ujio wako hapa duniani ni mpango kamili wa Mungu.

Pamoja na ukweli huo, wengi wetu hatujui maono wala karama Mungu alizotupa, hivyo kufanya watu wengi kuishi maisha ya ‘kubangaiza’, yaliyojaa malalamiko na kukata tamaa.

Hata hivyo, ukweli unabakia pale pale kwamba mafanikio yako yatategemea jinsi utakavyozitambua karama ulizopewa na Mungu na kuzifanyia kazi! Wengine hutambua maono na karama zao mapema na huwa baraka kwa wengi kwa muda mrefu.

Wengine hutambua maono na karama zao katikati ya maisha yao na kujikuta hawana muda wa kutosha kutumika. Na wengine hawatambui karama zao kabisa hadi wanapokufa. Maono mengi yamezikwa pamoja na waliokata tamaa.

Kutotambua maono mapema utafanana na mtu aliye kwenye chumba chenye giza akilaumu kukosekana kwa mwanga. Mtu huyu katika mazingira hayo ya giza hukata tamaa na kukubali hali hiyo kama sehemu ya maisha yake! Kumbe alichotakiwa kufanya ni kujua swichi ya taa iko wapi na kuiwasha.

Ili upate ushindi katika mchezo wowote ni lazima kwanza ujue kipawa na uwezo wako kabla ya kushindana. Mwenye karama ya kukimbia akiamua kucheza mpira wa miguu atajikuta hawezi na mwisho atakata tamaa na kujiona hafai.

Kumbe, kosa lake ni kutotambua karama yake. Vivyo hivyo katika maisha, tunajiingiza kufanya jambo ambalo ni nje ya mpango wa Mungu na tunaposhindwa tunakata tamaa ya maisha.

Jamii zetu nazo kwa kiasi kikubwa huchangia kutufanya tushindwe kutambua karama zetu. Huku kwetu Afrika kwa kiasi kikubwa hatuwatii moyo wale wenye vipawa. Nchi za wenzetu hasa Ulaya na Marekani wameweka utaratibu wa kutambua vipawa vya wanafunzi wakiwa bado shule za awali, utaratibu unaoendelea hadi wanapomaliza chuo!

Matokeo yake unapata vijana waliofahamu maono na karama zao mapema na huwa ni baraka kwa jamii na taifa kwa ujumla. Mfumo wetu wa elimu kwa kiasi kikubwa unachangia kuua vipawa na karama Mungu alizoweka kwetu.

Fikiria mwanafunzi kuanzia shule ya msingi anapatiwa masomo ambayo hayaendani na karama yake, kwa sababu hakuna utaratibu wa kutambua karama hizo mapema! Anaposhindwa baadhi ya masomo hukata tamaa na kuathirika kisaikolojia mapema, kumbe masomo aliyoshindwa sio karama yake! Mfumo wa aina hii wengi wamejikuta wanasoma hadi chuo na kufanya kazi ambazo siyo wito wao kabisa!

Ipo sababu nyingine ambayo ni kukatishwa tamaa na wengine. Hakuna mtu anayejipanga kwenda kumkatisha mtu mwingine tamaa. Mara nyingi wakatishaji tamaa huja kama wana wa nuru, washauri wema. Watakueleza kwa umakini kile wanachokielewa kuhusu unachotaka kufanya.

Watakupa sababu na mara nyingi ni za kitaalamu kabisa za kwa nini usifanye hicho ulichopanga. Mtu mmoja alisema unapotaka kufanya jambo waulize wataalamu kwanza, wakikwambia usifanye usibishane nao, wewe nenda kalifanye!

Maana yake ni nini? Watu wengi wanapokupa ushauri hutokana na yale waliyopitia, yaani uzoefu wao. Aliyepata msukosuko katika ndoa atakueleza jinsi wanaume walivyo wabaya na kukushauri usikubali kuolewa yasije yakakupata yaliyompata! Kumbe kuna ndoa nyingine nyingi tu maisha ni ya amani na mafanikio.

Mwingine atakushauri usikubali kukopa ili ufanye biashara au kilimo kwa sababu yeye alipokopa alishindwa kulipa deni. Zipo sababu nyingi zilizosababisha yeye kushindwa kulipa deni ingawa hatakueleza. Anachofanya ni kukukatisha tamaa akidhani anakutahadharisha!

Wakatishaji tamaa huhamisha uzoefu wa kushindwa kwao kwa wengine wakidhani wanasaidia. Watu hawa mara nyingi huwa ni wale ambao hawakutambua maono na karama Mungu alizowapa.

***Na walipoingia kufanya nje ya mpango wa Mungu na kushindwa, wanakuwa wataalamu wa ushauri. Ieleweke siyo kila anayekushauri lengo ni kukukatisha tamaa. Tukutane tena wiki ijayo. Una maoni, tuma ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Barabara ya Mwenge – Bunju inatakiwa kujengwa upya

HALI ya usafiri kwa barabara ya Bagamoyo kipande cha Tegeta hadi Bunju ni ya mateso kwa watumiaji wake kutokana na kuongezeka kwa watumiaji hali inayolazimu kukaa kwenye foleni kwa muda mrefu.

Unapotoka Mwenge kwenda Bagamoyo uwe na uhakika utapoteza muda mwingi katika kipande cha Tegeta hadi Bunju, jambo linalohitaji hatua za haraka.

Watumiaji wa barabara hii wameongezeka kutokana na vyombo vya usafiri kuongezeka kama magari, bajaji na pikipiki, vyote vikitumia barabara hiyo kwa namna ya tofauti. Pikipiki na bajaji, kwa mfano zinapenya kokote wanakoona kuna nafasi.

Magari hulazimika kubaki kwenye njia kuu kwa kuwa barabara hiyo ni nyembemba inatosheleza magari yanayokwenda na kurudi. Inapotokea kuna gari lililoharibika watu watasota kwa muda mrefu kwa kuwa hakuna njia mbadala ya kukuwezesha kuendelea na safari.

Barabara hiyo pia hutumiwa na mabasi ya mikoani yanayoanzia safari zake Kituo Kikuu cha Magufuli ambayo husimama kwenye vituo kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria.

Kutokana na ukubwa wa mabasi hayo ambayo yakisimama kituoni yanachukua nafasi kubwa, huku daladala nazo zinapakia na kushusha abiria pasipo kusogea kwenye vituo, hali iinayoendelea kuongeza foleni na kusababisha mateso kwa watumiaji wote.

Barabara hiyo pia inatumika kama mbadala kwa wanaosafiri kwenda mikoa ya Tanga, Moshi na Arusha. Pia watu binafsi huitumia sana kwa kuwa baada ya kuvuka eneo lenye msongamano huko mbele mtu anakwenda kwa haraka.

Kwa hali hii inaonyesha umuhimu wa barabara hii kiuchumi, pia inawezesha watu kuwahi kwenye shughuli nyingine za kijamii, inaonyesha umuhimu wa kuchukua hatua madhubuti kuifanya kuwa njia nne.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, alitunukiwa tuzo ya mjenzi bora wa miundombinu ya barabara na reli. Maana yake Tanzania tunafanya vizuri katika kuunganisha nchi na kufungua fursa za kiuchumi katika kukuza uchumi.

Kwa msingi huo, licha ya kazi nzuri iliyofanyika ikiwamo kupanua barabara ya Morogoro kutoka Ubungo hadi Kibaha, kumesaidia kumaliza tatizo la foleni na sasa shughuli za kiuchumi zimefunguka ukanda huo.

Hivyo basi, umuhimu wa kupanua barabara ya Bagamoyo haukwepeki kwa kuwa sasa imeelemewa vinginevyo watu watateseka na kuchukua muda mrefu ambao wangeutumia kufanya shughuli za maendeleo.

Kuna utafiti ulifanyika ukaonyesha foleni husababisha nchi kupoteza mamilioni ya fedha kwa kuwa watu wanakaa bila kwenda kuzalisha, wanachelewesha kazi na bidhaa zinashindwa kufika sokoni kwa wakati. Hali hiyo pia inasababisha madhara ya afya kwa watu kwa kuwa ofisini wanakaa muda mrefu na kwenye magari wanakaa muda mrefu.

Mathalani, kama mtu anafanya kazi Posta analazimika kuamka saa 10:00 alfajiri kila siku na kama anatoka kazini saa 9:00 alasiri, basi atafika nyumbani saa mbili au tatu usiku na haya yatakuwa maisha yake ya kila siku hali itakayomsababishia madhara kiafya.

Mara nyingi mji wa kiuchumi Dar es Salaam, ndio unakabiliwa na adha ya foleni kutokana na kuwa na watu wengi na shughuli nyingi. Maana yake ni lazima kuwa na ubunifu katika kukabiliana na foleni ambayo ni kikwazo.

Kama zilivyojengwa barabara za mzunguko kupunguza foleni ikiwamo ya Goba hadi Mbezi, basi tuendelee kuimarisha miundombinu mingine na ikiwezekana kwa njia ya Bagamoyo zijengwe njia mbadala zinatakazosaidia kupunguza msongamano na kuharakisha shughuli za kiuchumi.

Ni lazima kuchukua hatua madhubuti kumaliza tatizo la foleni ambalo ni kikwazo ikiwa barabara hiyo itajengwa kwa njia nne au sita kama ilivyo ya Kimara hadi Kibaha, itarahisisha kama ambavyo watumiaji wa njia ya Morogoro wanavyofurahia miundombinu hiyo na sasa shughuli za kimaendeleo zinaendelea kuimarika.

Bila kufanya hivyo ni kuendelea kuikosesha serikali mapato na kididimiza kipato cha mtu mmoja hadi mwingine.





Katika konogesha vazi la bwana harusi ni muhimu kuweka alama ya ua juu ya mfuko wa koti lake safi. Pichani ni baadhi ya mitindo mbalimbali ya maua inayopamba nguo za bwana harusi

# MITINDO



# 'ATHLEISURE' MCHANGANYIKO WA MAVAZI UNAOVUTIA

KUNA siku unatamani uende kazini mwisho wa wiki ukiwa na 'leggings' au 'tracksuit', kwa sababu unaona yatakupa wepesi zaidi.

Lakini ndoto yako inaweza kutimia kama utavaa mavazi mchanganyiko ya michezo 'Athleisure' ambayo yatakuwa na mwonekano wa kawaida.

Lengo la Athleisure ni kuvaa mavazi ya kimichezo sehemu zisizo za kimichezo, aina hii ya uvaaji imepata umaarufu kutokana na kupata raha zaidi.

Mara nyingi nguo hizi huvutika, kitambaa chake huwa laini na hupitisha hewa.

Nguo za michezo hutengenezwa katika namna ambayo huruhusu karaha nyingi, jambo ambalo limewafanya watu watamani kuvaa nguo hizi katika shughuli mbalimbali nje ya michezo.

Katika kuvaa Athleisure unatakiwa kuchanganya nguo za kimichezo na nguo za kawaida. Nguo za kimichezo ni kama leggings, tracksuit, sports bra, t-shirts, tank tops, shorts, joggers, sneakers (raba) na nguo za mazoezi ya kubana.

Ili kutengeneza mwonekano wa 'Athleisure' unapaswa kuvaa angalau vazi moja la kimichezo, hivyo unaweza kuvaa tracksuit na viatu virefu, unaweza kuvaa gauni na sneakers, au unaweza kuvaa suti, sneakers na kofia.

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**

# KARABATI NGOZI

## Papai, limao, sukari inatosha



Wiki iliyopita tulielezana namna ya kutumia njia za asili kurekebisha ngozi iliyoharibika na mionzi ya jua. Leo tunaendelea kuangalia aina nyingine ya njia ya kujitibu.

Limao na sukari

Mahitaji limao na sukari kijiko kikubwa kimoja.

Namna ya kufanya, kamua limao kupata maji yake kiwango cha kijiko kimoja na uchanganye sukari kwenye maji ya limao.

Tumia mchanganyiko huo kama scrub katika sehemu iliyoathiriwa kwa kusugua taratibu kwa dakika mbili hadi tatu kisha nawa na maji.

Fanya hivi mara kwa mara kupata matokea mazuri zaidi.

Apple cider vinega na baking soda

Mahitaji ni baking soda kijiko kimoja cha chai na vinega kijiko kimoja.

Namna ya kufanya, changanya baking soda na vinega kupata mchanganyiko ambao sio mzito sana.

Paka mchanganyiko huu kama scrub na subiri kwa dakika 5 hadi 10 halafu unawe. Tumia hii mara moja au mbili kwa wiki.

**Papai**

**Mahitaji, papai lililoiva.**

Namna ya kufanya, chukua papai menya halafu ulisage. Paka mchanganyiko huu sehemu husika na usubiri kwa dakika 15 hadi 20 kisha nawa kwa maji ya uvugu uvugu. Paka kila siku au mara kwa mara mpaka utakapopata matokeo yatakayo kuridhisha.

**Kiazi mviringo**

Mahitaji, kiazi mviringo kimoja.

Namna ya kufanya, kata kiazi katikati, kisha anza kusugua sehemu husika taratibu.

Mbali na njia hizi zilizotajwa, pia inashauriwa kutumia mafuta maalum (sunscreen) ili kuikinga ngozi kutokana na madhara ya mionzi ya jua.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# PIKA SAMBUSA MBOGA

SAMBUSA ni aina ya kitafunwa ambacho kinapendwa na watu wengi.

Idadi kubwa ya watu wamezoea kula sambusa za nyama na viazi, lakini leo tutaelekezana namna ya kupika sambusa za mboga.

**Mahitaji**

Viazi mviringo vitatu vilivyochemshwa kisha uvikate vipande vidogovidogo, njegere zilizochemshwa kidogo nusu kikombe, vitunguu viwili kata vipande vidogo, tangawizi nusu, pilipili mbili na bizari nusu kijiko.

Giligilani iliyosagwa kijiko kimoka, garam masala nusu kijiko, majani ya curry manne, juisi ya limau kijiko kimoja, mafuta kijiko kimoja cha kupikia, chumvi, karoti mbili, unga wa ngano vijiko vinne, ute wa yai na chapati au manda.

**Maelekezo**

Weka tangawizi, kitunguu saumu na pilipili. Twanga kwa pamoja hadi vilainike kisha hifadhi pembeni.

Bandika sufuria au kikaangio jikoni. Weka mafuta, yakipata moto weka, bizari na majani ya curry.

Pika kwa dakika 2 huku ukigeuza mara kwa mara. Weka mchanganyiko wa pilipili kisha pika hadi harufu ya kitunguu saumu na tangawizi ipotee.

Weka kitunguu maji, pika kwa dakika mbili kisha weka mboga yoyote ya majani utakayopenda.

Weka viazi ulaya, unga wa giligilani, bizari, garam masala na chumvi. Changanya vizuri mpaka viazi vichanganyikane na viungo vingine.

Punguza moto uwe wa wastani, pika kwa dakika tano huku ukikoroga taratibu.

Weka njegere na limau. Changanya vizuri kisha pika kwa dakika mbili hivi. Toa motoni na acha mboga zipoe kabisa.

Koroga unga wa ngano au ute wa yai, hii itakusaidia kufungia sambusa. Kata manda kwenye umbo la pembetatu kisha weka mboga mboga kiasi.

Anza kufunga ila ukifika mwisho paka ute wa yai au unga wa ngano uliokoroga. Inasaidia sambusa zisifunguke wakati wa kupika.

Bandika kikaango chenye mafuta jikoni. Mafuta yakipata moto anza kupika sambusa hadi zigeuke rangi na kua kahawia. Yatoe na hifadhi pembeni. Rudia hii hatua hadi sambusa zote ziive.

Sambusa zikishapoa zinakuwa tayari kwa kuliwa na familia yako.



# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Chumba cha kulala nacho kinahitaji kuwa nadhifu

UMARIDALI huficha umaskini. Huo ni msemo ambao hutumiwa na wahenga wa lugha ya Kiswahili kuonyesha umuhimu wa mtu kuwa nadhifu au msafi.

Umaridadi ambao tumeuzoea sana ni ule wa umahiri wa kujiweka safi katika uvaaji au kwa lugha ya kigeni 'smart' wakati wote bila kujali una kipato kikubwa au la.

Lakini leo nataka nikwambie kwamba mbali na umahiri wa kujiweka safi katika mwili, pia unaweza kufanywa hata katika nyumba hususani katika chuma cha kulala.

Asilimia kubwa tumejikuta tukikifanya chumba cha kulala kama sehemu ya kurundika vitu ovyo eti kwa sababu hapaonekani katika uso wa wageni kama ilivyo katika sebule.

Kuna vitu muhimu ambavyo vinapaswa kuzingatiwa ndani ya chumba ili kukifanya chenye mvuto, chenye afya na hata kuimarisha ustawi wa nyumba yako ikiwamo mpangilio wake.

Hakikisha chumba chako kinawekwa katika mpangilio unaovutia hasa kwa kuangalia ukubwa na namna chumba chako kilivyotengenezwa na hakikisha unajenga umbo katika kichwa chako namna unavyotaka vitu vyako vipangiliwe, na kuepuka kupanga vitu ovyo mradi.

Zingatia kuweka vitu ambavyo ni muhimu na vina kazi katika chumba chako na si kuweka kila kitu kwa sababu ukiweka vitu vingi ambavyo havina umuhimu kwanza chumba chako kitakosa hewa, kitakuwa na hewa nzito lakini pia kitapoteza mvuto.

Mbali na hivyo, chumba kinachokosa mpangilio mzuri au kujazwa vitu pasipo sababu, uwezekano wa kukifanyia usafi wa uhakika ni mdogo na kwa maana hiyo hatari ya kuhifadhi wadudu ni kubwa.

Hakikisha samani muhimu pekee ndizo zinawekwa ndani kwa mfano kitanda, kabati na 'dressing table' na kuhakikisha vinafanyiwa usafi mara kwa mara.

Kwa kitanda, zingatia kukifanyia usafi kila siku, si kutandika mashuka tu bali pia kuhakikisha unakikagua kila eneo na kufuta kabla ya kutandika mashuka yako.

Safisha kuanzia uvunguni, katika kila kona ya maungio yake na baada ya kujiridhisha kwamba umesafisha kila mahali bila kusahau kukagua chandarua kama kiko katika hali ya usafi, kukichomoa kwenye kitanda na kasha kutandika shuka zako.

Kumbuka kwamba inavutia zaidi na kukifanya chumba kionekane chenye mzuto zaidi unapotandika kitanda chako kwa kukilembesha kidogo, usikubali kukiweka kikavukikavu na unaweza kutumia shuka zako hizo unazozitumia kwa siku husika na hata kwa kutumia mito.

Kwa upande wa kabati, nalo vitu vinavyoekwa ndani yake vinatakiwa vipangiliwe vizuri, ili liwe 'smart' na lisiharibu mpangilio wa chumba.


Pia hakikisha nguo zako unazipangilia vizuri katika sehemu yake, na viatu sehemu yake kwa kabati zenye sehemu ya kuwekea viatu hivyo.

Si kupangilia tu, lakini kabati linapaswa kusafishwa ili lisipate 'ukungu' na kuharibu nguo zako na mwisho wa siku ukasababisha harufu kwenye nguo.

'Dressing table', nayo vile vile inahitaji kuwa katika mpangilio mzuri. Hakikisha vitu vinavyowekwa kwayo vinakuwa katika mpangilio mzuri ambao nao huvutia ukiwekwa vizuri. Ondoa kila kitu ambacho hakistahili kuweka hapo.



## Namna ya kusafisha 'oven' baada ya kutumia



CHOMBO cha oven kinatumika sana majumbani kwa ajili ya kupashia joto au kuokea vyakula.

Hata hivyo, oven pamoja na kurahisisha kazi za jikoni, lakini inahitaji matunzo mazuri ili idumu, ikiwamo usafi wa kila mara ndani na juu ya oven.

**JINSI KUSAFISHA**


1: Tumia baking soda kwa kusafishia oven. Koroga uji wa baking soda na maji pakaa kwenye oven yako. lache kwa usiku mzima. Halafu, pulizia vinegar kumalizia uchafu wa baking soda. Futa vizuri.

2: Asubuhi yake unasugua ndani tumia sponji, halafu futa kwa kitambaa safi laini. Muda huo unapulizia vinegar kwa kitambaa unachopangusia mpaka uchafu wa baking soda uishe wote. Utaona rangi ya kijivu na brauni imeondoka.

3: Baada ya kuloweka na baking soda, nakusugua kutoa uchafu, hapa unaangalia kama oven yako inatoka kioo utatoa utasafisha hakikisha pameng'aa.

4: Tumia maji ya uvuguvugu kuloweka zile chuma za kupikia kukata mafuta. Tia sabuni kali acha kwa dakika 15-20, kabla ya kusugua.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
MAKAMO HAYO BADO UNAOGOPA KUTEKWA!
TATIZO SIO MAKAMO, BALI KIMO CHANGU JE, NAFAA KUTEKWA?
JUKWAANI
!?
MWANA-SI-HASA
AHADI NZITO
UNATAKA NINI TENA BONGE LABWANA.. MKEO NIPO SAWA KILA IDARA
NAFIKIRIA 'MIRUZI' YA BARABARANI SIJUI KAMA LEO SIJAMNG'ATA MTU MDOMO!
SHOSTI SIHANGAIKI NA JITU LENYE AKILI TIMAMU LINALOJITOA FAHAMU!
KAMA WEWE UHANGAIKI UJUE WENZAKO WANA-MUHANGAIKIA WAKIMPATA HUMUONI!
ACHENI HIZO MADA TUFIKIRIE NAULI KAMA ITASHUKA
ISHUKE UMEIWEKEA NGAZI?
KONDA TANGAZA VITUO
VYA POLISI?
INAMAANA BIA ZA HUKU HAZINA KILEVI MPAKA UFUNGE SAFARI UKALEWE TABATA?
'ASHU-RA' ATAWATOA ROHO!
NAMNA HII ALAFU NILISIKIE JITU LINATANGAZA ETI NIMETEKWA! SKUBALI...
WATUACHE NA KIINUA MGONGO CHETU
KIBURUGWA
SINZA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIZIMIKA TUNANUNA, UKIWAKA TUNASHANGILIA...

# Kalonzo Musyoka azuiwa kugombea urais

**NAIROBI,** KENYA

KIONGOZI wa Chama cha Wiper, Kalonzo Musyoka, ameondolewa kushiriki katika kinyang'anyiro cha urais wa Kenya.

Uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika Agosti 9, mwaka huu.

Uamuzi wa kumwondoa Kilonzo, katika orodha ya watu wanaogombea nafasi ya urais imechukuliwa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka nchini humo (IEBC).

Tume hiyo imewaidhinisha wagombea 16 ambao watawasilisha nyaraka zao za uteuzi kuanzia jana.

Orodha hiyo ina wafuasi tisa wa vyama vya siasa na muungano, huku wagombea saba huru.

Wagombea wakuu ni Raila Odinga kutoka muungano wa Azimio la Umoja, na Naibu Rais William Ruto wa United Democratic Alliance.

Musyoka hakuwasilisha orodha ya wafuasi wake katika karatasi inayohitajika.

Yeye ni miongoni mwa wagombea wanne wa vyama vya kisiasa na wagombea binafsi tisa ambao walishindwa kukidhi matakwa ya IEBC ya wafuasi 48,000 angalau katika kaunti 24, ikiambatana na majina ya wafuasi na nakala za vitambulisho vyao vya kitaifa.

**BBC**




Polisi wakikabiliana na waandamanaji wanaompinga rais mpya wa Philippine na makamu wake nje ya ofisi ya Taasisi ya Haki ya Binadamu ya Human Rights, katika eneo la Quezon y, jijini Manila. **PICHA: REUTERS**

# Rais wa Ukraine akiri hali ngumu Donbas

## ■ Majeshi ya Russia yazidi kuteka miji

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amewataka wanajeshi wake wanaweza kujiondoa katika eneo la mashariki la Luhansk ikiwa wanataka kuepuka kukamatwa na vikosi vya Urusi.

Taarifa kutoka uwanja wa mapambano inaeleza wanajeshi wa Russia wameingia katika mji wa Severodonetsk, lakini Jeshi la Ukraine bado linazuia mashambulizi.

Wakati wa hotuba yake ya usiku, Rais Volodymyr Zelensky alisema Ukraine itaweka upinzani mkali kulikomboa eneo la Donbas.

Kila siku inayopita, inaonekana Russia inachukua hatua nyingine nje ya eneo la Ukraine.

Jana walidai kuchukua mji wa Lyman ambao ni muhimu kimkakati kutokana na hapo ndipo wapiganaji wanaoungwa mkono na Russia walianza kampeni yao miaka minane iliyopita.

Hata hivyo, miji ya Severodonetsk na Lysychansk katika eneo la Luhansk iko katika hatari ya kutekwa kutokana na kuzungukwa na majeshi ya Warussia.

Gavana wa mji huo, Sergai Hidai ambaye ameonekana hana mamlaka yoyote, alisema Warussia wanadhibiti karibu asilimia 95 ya mkoa wa Luhansk.

Alisema huenda vikosi vyake vikahitaji kurudi nyuma ili kuepuka kukamatwa.

Hata hivyo, Rais Zelenksy alisema kuwa Donbas itakuwa ya Kiukreni huko na hawatakuwa na mbadala wa bendera za nchi hiyo.

Russia yateka sehemu kubwa ya Lyman Wizara ya Ulinzi ya Uingereza imethibitishwa kuwa vikosi vya Urusi huenda vimeteka sehemu kubwa ya mji wa Lyman katika eneo la Donetsk.

Taarifa hiyo ilisema ushindi huo ni dalili ya hatua inayofuata ya mashambulizi dhidi ya Donbas.

Mji wa Lyman ni muhimu kimkakati kwa sababu lina miundombinu ya madaraja muhimu ya reli na barabara juu ya Mto Siverskyy Donets.

"Katika siku zijazo, vitengo vya Russia katika eneo hilo vina uwezekano wa kuweka kipaumbele kulazimisha kuvuka mto," wizara hiyo ilisema.

Ilisema lengo kuu la Russia inabaki kuchukua Sieverodonetsk ambayo iko eneo la Luhansk.

Ikiwa jiji hilo litaangukia mikononi mwa Russia itadhibiti eneo la Luhansk. Wengi wanaamini Rais Vladimir Putin anaweza kushikilia udhibiti wa Donbas kama ushindi katika vita hiyo.

**BBC**

# Polisi yalalamikiwa kuchelewa wakati wa shambulio Texas

**TEXAS,** MAREKANI

OFISA mkuu wa usalama nchini Marekani, Steven McCraw, amesema polisi walifanya uamuzi usio sahihi kwa kushindwa kuvamia darasa la shule ya msingi huko Uvalde, katika jimbo la Texas.

Katika tukio hilo kijana mwenye bunduki aliwaua watoto 19 na walimu wawili kwa kuwapiga risasi.

"Ikiwa nilifikiri ingesaidia, ningeomba msamaha," Steven McCraw alisema wakati wa mkutano na waandishi wa habari juzi.

Alisema maofisa walichelewa kuingia kwa sababu hawakuamini kuwa bado ufyatuaji risasi uliokuwa ukiendelea.

Hata hivyo, wanafunzi waliokuwa ndani ya shule walipiga simu nyingi wakiomba polisi waje.

McCraw alithibitisha kuwa kulikuwa na pengo la dakika 40 kutoka kwa kitengo cha polisi kuwasili katika Shule ya Msingi ya Robb, hadi walipoamua kuvamia darasa ambalo mtu mwenye bunduki alikuwa amejificha.

Ofisa mkuu kwenye eneo la tukio aliamua kungoja hadi msimamizi wa shule atakapofika na funguo kwa sababu walidhani kwamba hakuna mtoto ambaye yuko hatarini kwa wakati huo, au hakuna mtu anayeishi tena.

Picha za video zinazoonyesha wazazi waliokuwa wamechanganyikiwa nje ya shule hiyo wakifungwa pingu na polisi huku mtu mwenye bunduki akiwa bado ndani. Hali hiyo imesababisha kuongezeka kwa hasira ya umma na kutaka uchunguzi wa jinsi vyombo vya sheria vilishughulikia tukio hilo. Juzi, Gavana wa Texas Greg Abbott alisema kwamba amepotoshwa kuhusu habari fulani, ambayo alikuwa ameweka hadharani katika mkutano na waandishi wa habari mapema wiki hii.

"Kama kila mtu anavyojua, taarifa ambayo nilipewa haikuwa sahihi," alisema.

**BBC**

## MAKALA

# WAFANYE WATU WAISEMEE VIZURI OFISI ULIYOKO SASA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

KATIKA juma lililopita nilizungumzia mambo mbalimbali kuhusu utoaji wa huduma katika ofisi za umma na binafsi. Hii ni baada ya kuanza kuona na kusikia malalamiko kutoka kwa wale wanaopata huduma katika ofisi hizo kwamba sasa hawaheshimiwi na kukirimiwa vizuri kama wateja na watu muhimu sana katika ofisi.

Hali hiyo ilinifikirisha sana na nikajisema moyoni kwamba nitafuatilia nijue ukweli. Nililazimika kujipa kazi hiyo kwa sababu katika kila unaloambiwa kuna ukweli kiasi na uongo ndani yake. Kwa maana hiyo, niliahidi kwamba nitakwenda kutazama mambo kadhaa ambayo kiongozi wa ofisi akiyafanya yatamsaidia kufanya huduma zake ziwe nzuri kwa wateja wake.

Katika ofisi yoyote, kuna makundi makubwa mawili ambayo yanahitaji huduma kutoka kwa kiongozi wa ofisi. Kundi la kwanza ni wafanyakazi au watumishi wenzako na kundi la pili ni wale mnaowahudumia kwa pamoja kama ofisi. Mfano kama ni Rais wa nchi, una watumishi wenzako kama mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri. Pamoja na kwamba unaweza kuwa wewe ndiye unayewateua, baada ya uteuzi, mnapaswa kufanya kazi kama timu ili kuwahudumia kundi la pili ambalo ni wananchi.

Jambo la kwanza kabisa ni lazima kila mtu atambue kwamba pale alipo ndipo kula, kulala na vaa yake ilipo. Hatuishi ili tule bali tunakula ili tuishi. Kwa maana nyingine, chakula ni uhai na usipokula utakufa. Kama ndivyo, huwezi kudharau jambo linaloweza kuhatarisha maisha yako. Ule usemi wa kazi ni uhai ndiyo maana yake hiyo. Ukidharau wateja umedharau kazi yako kwa sababu hao ndio wanaokufanya uitwe mfanyakazi au mtumishi wa umma.

Nafahamu kuna aina mbalimbali za uongozi ambazo watu hujifunza wawapo katika nyanja mbalimbali za elimu lakini ukitaka ushindwe kabla hujaanza, ni kung'ang'ana na ulichojifunza darasani badala ya mazingira ya unapofanyia kazi, kuna mambo ya kisheria na taratibu zake hilo linajulikana lakini suala la kukarimu watu ili wafurahie huduma zako ofisini pamoja na kwamba linafundishwa wanaita 'customer care' huduma kwa mteja lakini bado linabakia kuwa utashi wa mtu binafsi.

Kuna mambo madogo madogo ambayo yanaweza kufanya ofisi yako kuwa sehemu ya kimbilio. Hivi hujawahi kusikia watu wanasema ukienda ofisi fulani ukimkuta yule jamaa huwa anahudumia vizuri sana, lakini ukimkuta fulani hata shida yako usiseme rudi? Lakini watu wote hawa wawili utakuta wana elimu inayofanana tena kwenye eneo la uongozi walifaulu kwa kiwango cha juu, sasa unajiuliza tatizo nini?

Mfano wewe ni bosi wa ofisi fulani asubuhi umeingia kazini unakuta kuna watu wanakusubiri mlangoni kwako. Hivi ukifika hapo ukawasalimia jamani habari za asubuhi na baada ya hapo ukaingia ofisini ukaanza kumsikiliza mmoja baada ya mwingine, unapungukiwa na nini? Unakuta watu wako ofisini kwako unaingia tu hakuna hata salamu, yaani umeanza ugomvi kabla ya kuwasikiliza.

Kuna wengine wanateuliwa vijana wadogo, anaingia mzee ofisini humsalimii! Kwani ukimwambia mzee wangu shikamoo na ukaomba umsikilize atachukuwa cheo chako? Unataka wazee wakusalimie na wakuite mzee kwa sababu unadhani madaraka yanakupa umri! Unafurahi kuitwa bosi na ukiitwa hivyo unajitutumua kama kakakuona kapotea njia au paka kaona mbwa!

Jambo muhimu litakalokufanya uwe mtu mwema sana ofisini ni kutambua kwamba ofisi uliyomo ni sawa na nyumba ya kupanga, yeyote anaweza kuingia na kutoka pamoja na kwamba kuna baadhi ya wapangaji huwa wanaishi kwenye nyumba za kupanga na baadaye kuwa kama ndiyo wenye nyumba na kwamba yeyote anayetaka kuingia pale lazima yeye ndiye aamue. Lakini hilo haliondoi ukweli kwamba nyumba si yako.

Sifa kubwa kiongozi anayotakiwa kuwa nayo ni uwezo mkubwa zaidi wa kuwasikiliza watu. Kumsikiliza mtu ni pamoja na kuacha shughuli zako wakati ukimsikiliza. Kuna baadhi ya ofisi ambazo ndiyo unaingia, unaweza kuingia wakati unaeleza shida yako unayemweleza ama anachati na simu au yuko kwenye kompyuta anaendelea na mambo yake huku akikwambia endelea na baada ya hapo anajibu kwa kifupi tu.

Kama unaona unazo shughuli nyingi za kufanya, tenga muda au siku maalumu ya kusikiliza wateja, lakini si unasikiliza huku unatafuna bigijii au unachati. Ni muhimu sana unaposikiliza maelezo ya mteja, kumwonyesha wazi kwamba unamsikiliza kwa kumtazama usoni wakati akizungumza wanasema. Hii itamfanya akuone unamjali na itakujengea picha nzuri kwa wateja wako.

Kuna wakati unaweza kuwa uko ofisini halafu nje kuna watu (wateja) wanakusubiri. Wengine walikuja toka saa 2:00 asubuhi wamekaa mpaka saa 10 jioni wamechoka halafu unatoka ofisini hata hutaki kujua kama wamehudumiwa au la. Unatoka unapanda gari huyo, wanabaki wanaulizana hivi si huyu kweli? Ushamba na woga

Unachotakiwa kufanya ni kuwasalimia na hata kuwapa pole kwa kusubiri na kama umeona pengine kuna mahali unawahi waambie tu kuwa umepata dharura au kuna mahali unawahi na hatimaye kuwapangia muda wa kukuona. Nakuhakikishia hata kama hawakupata huduma, watatoka pale wakiwa na amani kwamba inawezekana kweli muda umekubana huku wakiamini kwamba ungeweza kuwahudumia. Wataondoka kwa matumaini ya kupata huduma siku nyingine.

Kuwahudumia watu vizuri ni faida kwako kuliko ilivyo kwao kwa sababu wale wale ndio watakaofikisha sifa zako njema kwa wengine. Kama ni mtumishi wa umma, taarifa zitawafikia waliokuteua na pengine wataona wakupe nafasi ya juu zaidi. Kama umeajiriwa na sekta binafsi, soko lako litakuwa kubwa. Utatafutwa na wengi na mshahara utapanga wewe kwa sababu utagombaniwa. Hakuna mtu anaweza kuwa na ofisi halafu asimwajiri mtu anayesifika kwa huduma nzuri ofisini.

Kuna watu wako ndani ya ofisi wana mtazamo kwamba, nikifanya vizuri sifa atazipata bosi wangu. Si kweli kwani utakayesifika ni wewe na mwisho wa siku na wewe mbeleni unaweza kuwa na ofisi yako kupitia ofisi ya bosi wako baada ya sifa zako kufika kila kona. Hiyo inakufanya kujitangaza wewe. Umepewa nafasi hivyo jitangaze kwa sifa njema kwa watu. Wafanye watu wakusemee, usiseme ziache kazi na huduma zako ziseme zenyewe.

Haya ni sehemu ndogo tu ya mengi yaliyosalia katika kuhakikisha huduma ndani ya ofisi yako inaboreshwa na watu wanakufurahia wewe binafsi pamoja na huduma zako. Fanyia kazi haya machache ndani ya muda mfupi utaona mabadiliko ndani ya ofisi yako na watu wataisemea wewe utakaa kimya.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Nyimbo 'Dada Asha', 'Dezo Dezo', Wakongo nao waliziiga za Bongo



Na Adam Fungamwango

WIKI mbili zilizopita, tulikuwa na mada ya bendi za Watanzania kuiga nyimbo kutoka kwa Wakongomani iliyokuwa na kichwa cha habari 'Napenda Nipate Lau Nafasi', na nyimbo zilizoigwa toka Congo DR.'

Nilipata simu na meseji kutoka kwa wasomaji wengi niwape na nyimbo ambazo Wakongo nao waliziiga kutoka Tanzania kwa sababu nilieleza kuwa hata wao pia kuna nyimbo waliziiga.

Wengi walikuwa wanafahamu bendi za Kitanzania zilivyokuwa zikiiga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) lakini si wengi waliofahamu kuwa Wakongo nao walikuwa wanaiga.

Tuliangalia jinsi wimbo wa 'Napenda Nipate Lau Nafasi' wa Kilwa Jazz Band ulivyochukulikuwa kutoka kwenye wimbo wa 'Mokolo Nakokufa' wa African Fiesta, ukiimbwa na Tabu Ley Rochereau, mwanzoni mwa miaka ya 1960.

Kilwa Jazz hao hao, wakaiga wimbo mwingine wa TP OK Jazz, chini ya Franco Luambi Luanzo Makiadi ulioitwa 'Course au Pouvoir'. Dar Jazz nao wakaiga wimbo wa TP OK Jazz ya Franco uitwao 'Quatre Boutons', wao wakauita 'Mtoto Aacha kupiga Mayowe'.

Ndala Kasheba, akiwa na Orchestra Safari Sound mwanzoni mwa miaka ya 1980, alirekodi wimbo ulioitwa "Uliomba Tucheze' ambao aliuiga kutoka pia TP OK Jazz, utunzi wake Ntesa Dalientst uliitwa 'Bina Ngai na Respect', yaani cheza na mimi kwa nidhamu.

Hizo ni baadhi ya nyimbo nyingi ambazo wanamuziki kutoka Tanzania haijalishi ni Watanzania au Wakongomani waliziiga kutoka DRC, wakati huo ikiitwa Zaire. Sasa tunakuja kwa Wakongomani ambao nao pia waliiga.

Wimbo wa 'Dada Asha' uliopigwa na Tabora Jazz Band, uliigwa mara nyingi zaidi na bendi nyingi za Zaire wakati huo kwa mujibu wa Tabu Ley alipofanya ziara mwanzoni mwa miaka ya 1980, kwanza alishangaa sana kusikia wimbo huo ni wa Tanzania. Akasema kule kwao Zaire, bendi nyingi zinaupiga na zipo zilizourekodi pia.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, Soukous Stars ikiwa na kina Ngouma Lukito, Dally Kimoko, Lokassa ya Mbongo, Shimita Lukombo Nzambi na wengine waliurekodi wimbo huo, kwenye albamu yao ya 'Nairobi Night'.

Ni kundi hilo hilo na kwenye albamu hiyo hiyo, pia ulirekodiwa wimbo wa 'Western Jazz' uitwao 'Vigelegele' ambao ulipigwa na bendi hiyo mwaka 1973.

Kundi hilo ambalo pia lilikuwa na mwamuziki kama Saladin Ferreira ambaye wengi wanadhani ni Mkongomani, lakini huyu ni raia wa Afrika ya Kati, ambapo alizaliwa jijini Bangui, na ndiyo maana kwenye baadhi ya nyimbo zao ambazo amepiga solo, au rhythm, kuna vipande ambavyo wanamtaja 'Saladin, Saladin, mwana Bagui'.

Wengine ni Yondo Sister, Lucien Bokilo, Na Balou Canta. Hao ni baadhi tu ya wanamuziki wanaounda kundi hilo ambalo kwenye albamu hiyo hiyo ya 'Nairobi Night', pia walirekodi wimbo wa Western Jazz' albamu ya mwaka 1973, wimbo unaitwa 'Roza'.

Kundi hilo lilirekodi wimbo huo bila ridhaa ya bendi au watunzi wa nyimbo hizo, na hata walipofanya ziara nchini katikati ya miaka ya 1990, walipoulizwa walisema kuwa nyimbo hizo walizinunua nchini Kenya.

Hawakufahamu kuwa ni nyimbo zilizopigwa na bendi za Kitanzania, badala yake wakadhani kuwa zilikuwa za bendi za Kenya, na hata waliowapa ruhusa ya kutumia nyimbo hizo, hawakuwa wanamiliki hati miliki za nyimbo hizo walikuwa nchini humo.

Hawakupata tabu sana kwa nyimbo za Western Jazz kwa sababu bendi yenyewe ilishakufa na wanamuziki wengi kusambaratika, wengi wakiwa hawapigi tena muziki, lakini kwa wimbo wa 'Dada Asha' kazi walikuwa nayo, kwani mtunzi Shem Karenga akiwa bado yu hai, aliwakalia kooni.

Kwa ujanja wa Wakongomani walichofanya ni kumjumuisha kwenye kundi lao la Soukous Stars na kuanza kuzunguka naye nchi nzima, hii ikazima joto la kuendelea kudai haki zake, kwa sababu alikuwa anajilipa sasa ndani kwa ndani. Mwanamuziki Tshala Muana naye alipofanya ziara nchini Tanzania mwanzoni mwa miaka ya 1990, alikuwa akizunguka na bendi ya Zaita Musica iliyokuwa na wanamuziki wa Kitanzania na Kikongomani.

Alipoondoka mwanamama huyo akaenda kurekodi nyimbo mbili za bendi hiyo 'Dezo Dezo' na 'Kokola' ambazo zilitungwa na Ndala Kasheba.

Alichukua bila ridhaa yake, na hata mwisho wa uhai wa Kasheba alifanya kazi kubwa sana ya kufuatilia pesa zake za haki shirikishi, kwa sababu alishtaki nchini Ufaransa ambapo mwanamama huyo alikwenda kurekodia nyimbo hizo.

Kwa wale wanaifahamu bendi ya Zaita Musica, ina nyimbo hizo 'Dezo Dezo' na 'Kokola', ambazo zinaimbwa na Kasheba mwenyewe, na Tshala Muana naye anazo, yeye aliziiga na kuziboresha zaidi zikipigwa kisasa zaidi, ikichagizwa na ubora wa studio.

Kwa bahati nzuri kesi hiyo ilimalizika vizuri, ingawa Kasheba hakuweka wazi kama alipata pesa au walielewana tu na Mkongomani mwenzake Tshala Muana.

**Tuma meseji 0716 350534**

HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofikia umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

RISASI ilikwenda moja kwa moja kwenye kichwa cha mzee Sabri na kumrusha hatua kadhaa mbele. Mlio mkubwa wa bastola ulisababisha watu mbalimbali waliokuwa maeneo jirani waanze kukimbia ovyo bila ya kujua wanapokimbilia.

Hiyo ilimpa fursa nzuri, Prince kujichanganya, akijifanya na yeye ni mmoja kati ya watu waliohamanika na kusikia sauti kali ya mlio huo wa ghafla.

Moja kwa moja alikwenda hadi maeneo ya Amana, akaingia kwenye gari lake ambao alilipaki na kutokomea. Wala hakuhitaji kujua kama amekufa au la. Kwake kulenga shabaha ulikuwa ni mchezo mdogo sana.

Alianza kuwa mlenga shabaha akiwa na umri wa miaka minne tu, hivyo alikuwa na uhakika kuwa atampiga kichwani na hala hakuhitaji kupiga nyingine ya kuhakikisha kuwa amekufa. Moja tu ilimhakikisha kuwa imefumua ubongo. Kitu anbacho kwake ilikuwa mara ya kwanza kukihisi ni kuua binadamu.

Sasa shauku yake ilikuwa moja tu. Ilikuwa ni kujua mama yake ni nani na yupo wapi kama alivyoahidiwa na baba yake mzee Pokwa.

*********************************

"Kazi nzuri mwanangu. Lakini ndiyo kwanza imeanza. Kuna watu wanne wamebaki."

"Ambao nao wanatakiwa wauawe?"

"Ndiyo. Hawatakiwi kuishi duniani. Ni watu wabaya ambao kama wakiendelea kuishi ni hatari sana kwetu." Mzee Pokwa alikuwa akiongea na kijana wake siku moja baada kutekeleza mauaji aliyomwagiza.

"Nilikuwa na wasiwasi kama unaweza kuimudu, lakini mimi mwenyewe leo nimekisikia kifo kikitangazwa kwenye taarifa za habari za redio, televisheni na mitandao ya kijamii, hongera sana. Unahitaji zawadi gani kwa kazi hii tu ambayo umeifanya mwanangu Prince?"




**Mashamba yake maeneo ya Chanika Zingiziwa. Kwa bahati mbaya alipakana na watu wabaya. Wao baada ya kuona wazazi wake wamefariki walianza kulimega na kufanya kila aina ya vitimbi ambavyo vilionekana kabisa kuwa wataka kulichukuwa."**

Alimtazama baba yake, halafu akajibu kwa sauti ya chini "Sihitaji chochote zaidi ya ulivyonieleza juzi kuwa nilifanikiwa hili utanieleza juu ya mama yangu na kwa nini naishi maisha haya ya upweke.

"Maisha yote unayoishi, ingawa unaishi kwenye nyumba nzuri, unapata kila kitu, baba yako nina mali nyingi, lakini upweke huu tulionao mimi na wewe, unasababishwa na watu kama hawa. Unasababishwa na mzee Sabri na wenzake. Mwanangu nenda kwanza kammalize. Ukifanikiwa nitajua sasa umekuwa. Umekuwa mkubwa, na hapo nitakueleza kila kitu." Prince alikumbuka maneno ya baba yake aliyomwambia juzi.

Taratibu mzee Pokwa aliuweka mkoba wake mezani na kuanza kuchambua baadhi ya vitu. Alitoa picha moja na kumkabidhi Prince.

"Huyu naye nikamuue?" Akauliza baada ya kuiangalia picha ya mwanamke mmoja mrembo asiyezidi miaka 30.

Mzee Pokwa alitabasamu kidogo, lakini akarudia kwenye hali yake ya kawaida.

"Huyu ndiye mama yako mzazi." Aliongea kwa sauti nzito, akionekana kuwa na uhakika na anachokiongea.

Ilikuwa ni mara ya kwanza Prince kuiona picha inayosemekana kuwa ni ya mama yake mzazi.

Aliitazama mwa dakika 10 picha ya mwanamke aliyeambiwa kuwa ni mama yake mzazi. Ilikuwa ni mara ya kwanza kuiona. Machozi yalimlengalenga. Hakika hata mwenyewe alipoitazama, akikiri kuwa mama yake angeweza kushinda kama si kuwa ndani ya washindi watano wa mwanzo kwenye shindano ya Miss Tanzania.

Baada ya kuondosha macho yake kwenye picha akayahamishia kwa baba yake.

Ni kama alikuwa anamuuliza "Enhee lete habari, aliishi vipi na ilikuwaje hadi akafariki?"

"Nilimuona mama yako, akiwa msichana mdogo sana, miaka 20 tu, nikaishi naye vizuri tu. Bahati nzuri wazazi wake walikuwa na uwezo, kwa hiyo walipofariki wamuachia nyumba kadhaa na mashamba.

Mashamba yake maeneo ya Chanika Zingiziwa. Kwa bahati mbaya alipakana na watu wabaya. Wao baada ya kuona wazazi wake wamefariki walianza kulimega na kufanya kila aina ya vitimbi ambavyo vilionekana kabisa kuwa wataka kulichukuwa."

Prince alikuwa akisikiliza kwa makini sana historia ya mama yake ambayo hakupata kuisikia.

"Samahani kwanza baba." Alimkatisha, halafu akendelea "Nilizaliwa peke yangu, au nilikuwa na ndugu zangu?"

"Hapana mwanangu." Akajibu, halafu akawa kama mtu anayefikiri kitu hivi "Wewe ndiye alikuwa wa kwanza kuzaliwa. Mama yako alifariki ukiwa na miaka miwili tu. Na kwa bahati mbaya alifariki akiwa na ujauzito wa mwezi mmoja. Ina maana walikufa akiwa na kiumbe, ambaye ni mdogo wako aliyekuwa tumboni."

"Enheee baba alifariki vipi?"

"Aliuawa."

"Na nani?"

"Ni hawa ambao leo nakwambia ukawaue."

"Kisa?"

"Ni hayo mashamba ya urithi. Wao walimuona mama yako ni mtoto mdogo tu, kwani hiyo walichofanya majirani zake hao, wakagawana mashamba. Wakatengeneza nyaraka feki kuonyesha kuwa baba na mama yake waliwauzia. Ukweli ni kwamba mama yako alikuwa na nyaraka halisi."

Wakati mzee Pokwa anaongea maneno hayo, macho ya Prince akahamia tena kwenye picha ya mama yake.

"Ilikuwaje sasa mpaka akauawa?" Akauliza. huku akiiweka sasa picha mezani.

"Ni kwamba aliwaambia kuwa atawashtaki kwa sababu nyaraka halisi anazo. Na siku aliyokuwa anakwenda kwa mwanasheria wake akiwa na nyaraka za mashamba kwenye mkoba wake, gari alilopanda akiwa na dereva wake lilivamiwa na magari mawili. Moja lilisimama mbele na lingine nyuma. Dereva aliposhuka kuuliza imekuwaje, alipigwa risasi, mmoja aliyekuwa kwenye gari la nyuma naye alitoka na kufungua mlango, akampiga risasi ya kichwa mama yako."

Wote walikaa kimya kwa muda wa dakika nzima hivi. Kila mmoja alikuwa anatafakari.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

# JUAN, BEN POL WAILETA 'VAMONOS' KIMATAIFA



NGOMA mpya ya mwanamuziki nchini Ujerumani Juan Daniel akimshirikisha Ben Pol, inayoitwa Vamonos imeachiwa rasmi ikiwa na moto wa aina yake.

Wimbo huo ambao umeimbwa kwa lugha mbili ya Kiswahili na Kijerumani, imeonekana kuwavutia mashabiki wa muziki kutokana na aina ya muziki wake.

Kwenye video anaonekana Ben Pol na Juan wakiimba na kucheza pamoja na watoto wa Kiafrika katika mazingira halisi ya kijijini.

# Malaika amwomba Rais Samia kuongeza walimu wa kike

Msanii wa kike wa muziki wa Bongofleva, Diana Exavery maarufu Malaika, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuongeza idadi ya walimu wa kike katika shule za sekondari nchini ili kuwasaidia kupata watu sahihi wa kuwaeleza changamoto zao.

Msanii huyo ambaye alikuwa ni mmoja wa waalikwa katika maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama Duniani jana, katika Shule ya Sekondari Tambaza na kudhaminiwa na Taasisi ya Gusa Initiative, amesema zipo shule ambazo zina upungufu mkubwa wa walimu wa kike huku zingine zikiwa hazina kabisa jambo ambalo huwawia vigumu wanafunzi wa kike kupata mahali pa kueleza shida zao.

"Kuna shule moja nilishawahi kuitembelea huko Karagwe ilikuwa ni katika kuelemisha masuala ya hedhi salama na kulikuwa hakuna mwalimu wa kike hata mmoja."

"Katika kuuliza tukaambiwa kwamba ni kutokana na umbali kwa hiyo kuna haja ya kuliangalia suala hili kwa jicho jingine na tunamwamini mama yetu Samia Suluhu," amesema Malaika.

Mwanzilishi wa Gusa Initiative, Queen Johnson, ameeleza taasisi hiyo itagawa taulo za kike elfu moja kwa wanafunzi wa shule hiyo ili kuwafanya watabasamu wanapokuwa katika siku zao.

"Hili ni kongamano letu la kwanza kama Gusa hapa Tambaza tuliona ni bora tuungane na wanafunzi hawa na pia tutagawa taulo za kike kuanzia elfu moja na kuendelea," amesema Queen.

Amesema taasisi hiyo iliona ni vyema kuwashika mkono watoto wa kike kwa kuwapatia taulo hizo ili kuwapa nafuu ya maisha wanapokuwa shuleni na kuweza kumudu masomo yao bila usumbufu.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEVES NA MAN
KLABU ya Manchester United wako mbioni kufanya harakati za mwisho kumsajili mshambuliaji wa Wolves, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, ingawa wanakabiliwa na ushindani kutoka Barcelona. ***(Sun)***

### NUNEZ BEI JUU
MANCHESTER United wanahofia gharama za uhamisho wa Darwin Nunez huku Benfica wakiwa wameiambia United itawagharimu takriban pauni milioni 100 kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 22. ***(Star)***

### TORRES NAYE ATAKIWA
MANCHESTER United pia imezungumza na kocha wake mpya, Erik ten Hag kuhusu uwezekano wa kumsajili mlinzi wa Villarreal, Pau Torres mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Manchester Evening)***

### CHELSEA MABEKI WANNE
CHELSEA wanatarajiwa kusajili mabeki kwa bajeti yao ya uhamisho ya pauni milioni 200, huku wanne wakitarajiwa kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto. Wanaweza kushindana na Manchester City na Tottenham kwa beki wa kushoto wa Brighton mwenye thamani ya pauni milioni 45, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 23, wakati winga wa RB Leipzig Mfaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, akiwa mlengwa mwingine. ***(Sun)***

### MANE KUMRITHI LEWANDOWSKI
LIVERPOOL itapokea takribani pauni milioni 25 kwa uhamisho wa Sadio Mane kwenda Bayern Munich, huku mshambuliaji huyo wa Senegal mwenye umri wa miaka 30, akipangwa kuchukua nafasi ya Robert Lewandowski. ***(L'Equipe)***

### SUAREZ HUYO VILLA
KLABU ya Aston Villa inaangalia uwezekano wa kumsajili Luis Suarez mwenye umri wa miaka 35, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuachwa na Atletico Madrid. Mshambuliaji huyo wa Uruguay ni mchezaji mwenzake wa zamani na kocha wa sasa wa Villa, Steven Gerrard. ***(Telegraph)***

### NEYMAR KUUZWA
KLABU ya Paris St-Germain inamfanya Neymar mwenye umri wa miaka 30, kupatikana kwa uhamisho msimu huu wa joto. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alijiunga na klabu hiyo ya Ufaransa kwa ada ya rekodi ya dunia ya euro milioni 222 mwaka 2017, lakini ameonekana mara chache kutokana na majeraha ya mara kwa mara. ***(ESPN)***

### PEPE ANUKIA PSG
PARIS St-Germain wamepewa ofa ya kumsajili winga wa Arsenal na Ivory Coast, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 26. ***(FootMercato)***

### CORNET AVUTIA WENGI
MSHAMBULIAJI wa Burnley na Ivory Coast, Maxwel Cornet mwenye umri wa miaka 25 anawavutia wengi baada ya timu yake kushushwa daraja. Klabu za West Ham, Newcastle, Brighton, Everton, Wolves, Crystal Palace, Leicester na Fulham ni miongoni mwa klabu zilizofanya mawasiliano na wawakilishi wa Cornet. ***(90 min)***

### DIABY ATAKIWA
KLABU ya Newcastle inataka kumwongeza winga wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 22 kwenye safu yao ya ushambuliaji msimu ujao. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# HATIMA YA JESUS CITY HAIELEWEKI

Wakala wake athibitisha kupokea ofa kibao kutoka klabu kubwa, lakini asema watakaa na kuamua wapi atacheza msimu ujao na...

**MANCHESTER, England**

WAKALA wa fowadi wa Manchester City, Gabriel Jesus amethibitisha kuwa wanatathmini ofa zote zilizotolewa kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu mustakabali wa Mbrazil huyo.

Jesus amebakiwa na zaidi ya miezi 12 katika mkataba wake wa sasa pale Etihad na anakabiliwa na mustakabali usio na uhakika baada ya mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England kumsajili Erling Haaland na Julian Alvarez.

Kwa mujibu wa 90min, Arsenal na Tottenham wamewasiliana na kambi ya Jesus ili kuwania saini yake, ingawa City haijakata tamaa ya kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 na Kocha Pep Guardiola amweweka wazi kuwa hataki Jesus aondoke.

Wakala wa Jesus, Marcelo Pettinati, amekuwa akifanya kazi ya kutafuta chaguo bora kwa mteja wake.

Kwa sasa tunaelewa ofa zote zinazotolewa, kwa hiyo sasa sio wakati wa kusema chochote, "alisema Pettinati akinukuliwa na Sky Sport.

"Mambo yatasonga mbele baada ya muda wake na timu ya taifa." Baada ya kushinda taji la Ligi Kuu akiwa na City, Jesus alifichua kwamba ameiarifu City kuhusu mustakabali wake ndani ya klabu hiyo.

Aliiambia ESPN: "Kuhusu mustakabali wangu, bado haijulikani. Nina mkataba na City na tayari nimeeleza nia yangu kwa watu wa City na kwa wakala wangu. Nina kile ninachotaka kichwani.

"Baada ya likizo, nitaamua kuhusu maisha yangu ya baadaye."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
PYRAMIDS
VERSUS
AL MASRY CLUB
1 | 1.40
X | 4.48
2 | 7.17

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LAUTARO: DYBALA ATACHEZA ANAKOPAPENDA



**BUENOS AIRES, Argentina**

LAURATO Martinez hajui ni wapi fowadi anayehusishwa na Inter Milan, Paulo Dybala atacheza msimu ujao, lakini anatumaini atakuwa sehemu "atakayokuwa na furaha".

Mkataba wa Dybala ndani ya Juventus unamalizika mwezi huu, na hivyo kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaotafutwa sana hasa kutokana na kuwa huru.

Ripoti zilizoenea zimeeleza kwamba, ana uwezekano mkubwa wa kuungana na mchezaji mwenzake wa Argentina, Martinez pale Inter - ingawa mshambuliaji huyo wa Nerazzurri pia anahusishwa na uvumi wa kuondoka.

Lakini wakati wawili hao wakielekea kwenye majukumu ya timu ya taifa, Martinez amesisitiza kwamba, mustakabali wa klabu ya Dybala umewekwa pembeni.

"Hatukugusia suala hilo," alisema Martinez akiiambia TyC Sports.

"Tunazungumza mambo mengi, kuhusu hali yake na kila kitu, lakini sasa anafikiria kuhusu timu ya taifa.

"Mustakabali wake utaamuliwa baada ya michezo hii itakapokamilika.

"Ni mchezaji mwenye ubora, utu na ninatumaini atacheza pale anapojisikia vizuri zaidi, pale anapofurahia."

Martinez pia anatarajia kuichezea Argentina kwa mara ya kwanza kwenye Kombe la Dunia kule Qatar baadaye mwaka huu la kwanza katika maisha yake ya soka na timu ya taifa.

"(Kombe la Dunia) ni ndoto ambayo nimekuwa nayo tangu utotoni," alisema Martinez.

"Pamoja na familia yangu, mimi huzungumza kila mara kuhusu hili - wote ni mashabiki wa soka.

"Ikiwa nitafikiria sasa juu ya kile kinachoweza kutokea, wasiwasi huja kwangu. Natumaini tunaweza kuacha hisia nzuri.

"Hizi ni ndoto ambazo huwa unazo kila mara. Kwanza ndoto zako ni kucheza kila wakati. Leo imebaki miezi kadhaa kabla ya kombe la dunia."

# Chelsea yajiandaa kumnasa Dembele

**LONDON, England**

CHELSEA wanajiamini kwamba, wanaweza kunufaika na hali ya sintofahamu kuhusu mustakabali wa Ousmane Dembele kwa kutofikia makubaliano na Barcelona na wanaweza kumchukua pale Stamford Bridge, kwa mujibu wa 90min.

Mkataba wa winga huyo wa Barcelona unamalizika mwishoni mwa Juni.

Aliwekwa sokoni Januari na mazungumzo ya mkataba mpya yalikwama kutokana na mahitaji yake ya mshahara, lakini hatimaye alibaki Camp Nou kwa nusu ya pili ya msimu.

Mazungumzo yameanza tena na inaelewa kuwa Barcelona wamekaribia kufikia matarajio makubwa ya Dembele, ingawa bado hawana imani kama atakubali kusaini mkataba mpya.

Rais wa Barcelona, Joan Laporta amelazimika kuweka muda wa mwisho kwa mchezaji huyo kufanya uamuzi wake.

Paris Saint-Germain pia wamewasilisha ofa mezani kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Pendekezo la PSG lilikuwa chini ya mkurugenzi wa michezo Leonardo, lakini anatarajiwa kufutwa kazi na nafasi yake kuchukuliwa na Luis Campos - ambaye si miongoni mwa watu wanaomvutia Dembele.

Hilo linaweza kuwapa Chelsea nafasi ya moja kwa moja kumsajili mchezaji huyo ambaye atakuwa huru hivi karibuni.

The Blues walipanga kuanza mazungumzo na Mfaransa huyo mara tu Todd Boehly atakapowekwa rasmi kama mmiliki wao mpya.

Kocha Mkuu Thomas Tuchel anataka kujiimarisha katika maeneo kadhaa, ikiwa ni pamoja na safu ya ushambuliaji, ambapo mustakabali wa Timo Werner na Hakim Ziyech haujulikani na Dembele pia anaaminika kutaka kuhamia London.

Lakini vyanzo vingine vimebainisha kuwa Bayern Munich nayo inamtaka mchezaji huyo.

Dembele sasa anajiandaa kuingia mwezi wa mwisho wa mkataba wake na Barcelona na mustakabali wake haujakaribia kutatuliwa, na wakala wake, Moussa Sissoko amethibitisha mteja wake 'amebaki huru' kwa kila jambo.

"Mustakabali wa Ousmane unabaki wazi na hatutaingia katika uvumi usioisha," alisema Sissoko akiiambia Goal.

"Wakati utakapowadia, Ousmane atachukua chaguo bora zaidi. Sisi tumekuwa tukiheshimu sana klabu zote na tutaendelea vivyo hivyo mradi tu mchakato unaendelea.

"Wakati ni sahihi kufanya uamuzi, Ousmane atazingatia ni chaguo gani bora kwa maisha yake ya baadaye."

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

***
Mwisho.

# RAIS SAMIA KULIPOKEA KOMBE LA DUNIA

**Na Saada Akida**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan atakuwa mgeni rasmi katika ziara ya kupokea Kombe halisi la Dunia (Fifa World cup Trophy Tour) linalotarajia kufika nchini Mei 31, mwaka huu.

Kombe hilo ambalo linaletwa na Kampuni ya kinywaji cha Coca Cola ambayo pia inamleta aliyewahi kuwa nguli wa Barcelona FC na Chelsea, Juliano Belletti.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, alisema kombe hilo litawasili nchini Jumanne na Rais Samia atakuwa mgeni rasmi katika hafla ya kulipokea.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi nne ikiwamo Kenya, Ethiopia na Afrika Kusini zilizopata nafasi ya kutembelewa na kombe hilo ambalo ni hamasa kubwa kwa Taifa kupigania kufanikiwa kutafuta nafasi ya siku moja kufuzu kucheza Kombe la Dunia.

"Ujio wa kombe hilo ni hamasa kwa Tanzania kuhakikisha tunakuwa tayari kwa timu yetu ya soka (Taifa Stars) tunapata nafasi ya kushiriki michuano hiyo siku moja," alisema katibu huyo.

Alisema katika hafla hiyo Rais Samia ataungana na baadhi ya wawakilishi na wadau wa michezo kutoa nasaha zake katika sekta ya michezo.

Abbas alisema baada ya hafla hiyo, Juni Mosi, mwaka huu litapelekwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa ajili kutoa fursa Watanzania na wananchi kupiga picha na kombe hilo.

Naye Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya Coca-Cola, Josephine Msalilwa, alisema Juni Mosi itakuwa siku ya Watanzania kupiga picha na atakuwapo mchezaji nguli aliyewahi kucheza Kombe la Dunia, Belletti ambaye amelileta kombe hilo.

"Mbali na kupiga picha, lakini katika ziara ya Kombe la Dunia kutakuwa na burudani mbalimbali kwa ajili ya Watanzania ambao watakuja kupiga picha ikiwa ni kumbukumbu zao katika maisha," alisema Josephine.

# Coastal yaipania Azam leo



Wachezaji wa Azam FC, Sospeter Bajana (kushoto) na golikipa wake wakifanya mazoezi ya kujiandaa na mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Coastal Union utakaopigwa leo Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha. **PICHA: AZAM**

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Coastal Union imesema itashuka dimbani katika mchezo wa nusu fainali ya pili ya mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya Azam FC, huku akimkosa mchezaji wake, Victor Kapan.

Nusu fainali ya kwanza ya kombe hilo ilipigwa jana kati ya Yanga na Simba kwenye uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha mkuu wa Klabu hiyo, Juma Mgunda alisema kuwa wamejipanga vizuri kukutana na timu ya Azam licha ya kukosekana kwa mchezaji huyo.

"Kwa upande wetu tumejipanga vizuri katika mchezo huo ambao nina amini tutafanya vizuri," alisema Mgunda.

Kocha huyo alisema licha ya kumkosa mchezaji huyo hakuna kilichoharibika kwani wana wachezaji wengi wazuri.

"Hata akikosekana mchezaji wetu huyo hakuna kitakachoharibika kutokana na maandalizi ya muda mrefu tuliyoyafanya," alisema.

Aliomba mashabiki wao wajitokeze kwa wingi kuwapa sapoti kwani lazima waingie fainali.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 29/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4375 | Solihull Moors vs Chesterfield | 2.24 | 3.40 | 2.91 |
| 16:00 | 4580 | Hifk vs Honka | 4.57 | 3.45 | 1.69 |
| 16:00 | 4620 | Djurgardens IF vs Varbergs Bois | 1.39 | 4.28 | 6.81 |
| 16:00 | 4872 | Degerfors vs Malmo | 5.07 | 4.29 | 1.49 |
| 17:00 | 1620 | Coca Cola vs Eastern Company SC | 1.34 | 4.70 | 9.00 |
| 17:00 | 3207 | US Quevilly Rouen vs Villefranche Sur Saone | 2.09 | 3.12 | 3.56 |
| 17:00 | 3644 | Spartak Moscow vs Dinamo Moscow | 2.76 | 3.10 | 2.40 |
| 17:15 | 1764 | Levadia Tallinn vs Flora Tallinn | 2.95 | 3.15 | 2.43 |
| 17:30 | 5359 | FC Luzern vs FC Schaffhausen | 1.63 | 4.10 | 4.60 |
| 18:00 | 5375 | Istanbulspor vs Erzurum BB | 2.00 | 3.35 | 3.31 |
| 18:30 | 2263 | Huddersfield vs Nottingham | 3.37 | 3.17 | 2.14 |
| 18:30 | 2341 | IFK Varnamo vs Hammarby | 3.90 | 3.46 | 1.80 |
| 18:30 | 2746 | Helsingborg vs AIK Football | 5.43 | 3.68 | 1.55 |
| 18:30 | 3307 | Kerho 07 vs IF Gnistan | 2.37 | 3.36 | 2.63 |
| 18:30 | 3334 | PK-35 vs MP Mikkeli | 2.16 | 3.40 | 2.92 |
| 18:30 | 3761 | FF Jaro vs TPS Turku | 2.43 | 3.17 | 2.68 |
| 18:30 | 3836 | Pif Jalkapallo vs Japs | 2.37 | 3.36 | 2.63 |
| 18:30 | 4500 | IFK Mariehamn vs VPS Vaasa | 2.26 | 3.22 | 2.88 |
| 19:00 | 1015 | Molde vs Bodo Glimt | 2.22 | 3.59 | 2.89 |
| 19:00 | 1042 | Jerv vs Sarpsborg | 3.49 | 3.39 | 2.03 |
| 19:00 | 1219 | Fram Reykjavik vs Valur | 4.75 | 4.07 | 1.55 |
| 19:00 | 1366 | Pd Santa Eulalia vs Real Murcia | 3.11 | 3.16 | 2.17 |
| 19:00 | 1451 | ADO Den Haag vs SBV Excelsior | 2.17 | 3.41 | 3.06 |
| 19:00 | 1616 | Merida UD vs CD Teruel | 2.16 | 3.16 | 3.11 |
| 19:00 | 2055 | Haugesund vs Aalesunds | 2.21 | 3.48 | 2.98 |
| 19:00 | 4704 | Covilha vs Alverca Futebol | 2.10 | 3.35 | 3.35 |
| 19:30 | 4630 | Pyramids vs Al Masry Club | 1.40 | 4.48 | 7.17 |
| 19:30 | 5152 | Vikingur Reykjavik vs KA Akureyri | 1.91 | 3.64 | 3.30 |
| 20:00 | 1535 | IA Akranes vs Keflavik IF | 2.23 | 3.60 | 2.68 |
| 20:00 | 3410 | Padova vs Catanzaro | 2.12 | 3.15 | 3.60 |
| 20:00 | 5453 | Stjarnan vs Vestmannaeyjar | 1.65 | 3.99 | 4.09 |
| 21:00 | 1704 | Tenerife vs FC Cartagena | 1.50 | 4.17 | 5.76 |
| 21:00 | 2226 | Alcorcon vs Eibar | 7.94 | 4.57 | 1.36 |
| 21:00 | 2539 | Real Oviedo vs UD Ibiza Eivissa | 1.56 | 3.96 | 5.34 |
| 21:00 | 2907 | Valladolid vs Huesca | 1.34 | 4.98 | 7.37 |
| 21:00 | 2977 | Valerenga vs Rosenborg | 2.24 | 3.40 | 3.00 |
| 21:00 | 3225 | Burgos vs Girona | 3.75 | 3.01 | 2.08 |
| 21:00 | 3390 | Sporting Gijon vs Las Palmas UD | 5.35 | 3.51 | 1.64 |
| 21:00 | 4406 | Dinamo Bucuresti vs Universitatea Cluj | 1.50 | 4.06 | 5.94 |
| 21:00 | 5640 | Leganes vs Almeria | 4.65 | 3.61 | 1.70 |
| 21:30 | 1989 | Palermo vs Feralpisalo | 1.82 | 3.45 | 4.40 |
| 21:30 | 4832 | Moreirense vs GD Chaves | 1.89 | 3.28 | 4.17 |
| 21:30 | 5563 | Pisa vs Monza | 2.38 | 2.93 | 3.13 |
| 21:45 | 1531 | Korona Kielce vs Chrobry Glogow | 2.16 | 3.20 | 3.40 |
| 22:00 | 1031 | Santos vs Palmeiras | 3.79 | 3.21 | 1.91 |
| 22:00 | 1785 | Vila Nova GO vs Gremio | 3.35 | 2.92 | 2.18 |
| 22:00 | 3238 | Coritiba vs Botafogo RJ | 2.35 | 3.01 | 2.92 |
| 23:00 | 5015 | Caracas FC vs Ucv FC | 1.73 | 3.30 | 4.57 |
| 23:30 | 2849 | Defensor Sporting vs Deportivo Maldonado | 1.97 | 3.26 | 3.50 |
| 23:30 | 5675 | FBC Melgar vs Universitario | 1.48 | 4.10 | 5.47 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Mei 29, 2022
Nipashe



Hatima ya Jesus City haieleweki UKURASA 21




Mshambuliaji wa Yanga, Heritie Makambo, akiwania mpira na mlinzi wa Simba, Joash Onyango wakati wa mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA baina ya timu hizo, uliopigwa jana Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza. Yanga ilishinda 1-0. **PICHA: YANGA**

## Rais kulipokea Kombe la Dunia

**Na Saada Akida**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan atakuwa mgeni rasmi katika ziara ya kupokea Kombe halisi la Dunia (Fifa World cup Trophy...



HABARI UK 23

# YANGA MBABE

...Yaivua ubingwa wa FA Simba na kutinga fainali kwenye mechi kali iliyofanya kila timu kumiliki kipindi kimoja, shuti la Fei Toto gumzo kila kona na...

**Na Adam Fungamwango**

SHUTI kali la umbali wa takriban mita 35 lililopigwa na Feisal Salum 'Fei Toto' dakika ya 25, liliipa Yanga ushindi wa bao 1-0 dhidi ya watani zao wa jadi Simba na kuwavua rasmi ubingwa na Kombe la FA msimu huu.

Bao hilo pekee kwenye mechi ya nusu fainali ya michuano hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza uliofurika maelfu ya watazamaji, limeifanya Simba kuelekea kupoteza makombe yote mawili msimu huu, likiwamo la Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo ni kama vile wameshalipoteza.

Ulikuwa ni msimu mbaya kwa Simba, kwani ilichofanikiwa kuchukua ni Kombe la Mapinduzi ililolipata mwanzoni mwa mwaka huu kwa kuifunga Azam FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Ni ushindi ambao umeifanya Yanga kulipiza kisasi cha kufungwa mechi ya fainali ya kombe hilo msimu uliopita kwenye Uwanja wa Tanganyika, Kigoma Julai 25 mwaka jana, Simba ikishinda 1-0.

Yanga pia imelipa kisasi cha kufungwa mechi ya nusu fainali ya michuano hiyo misimu miwili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, iliponyukwa 4-1, Julai 12, 2020.

Ni mechi iliyoamua nani mbabe kati yao msimu huu, kwani kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu zote mbili walitoka suluhu.

Zilikutana mara ya kwanza mzunguko wa kwanza Desemba 11 mwaka jana na kutoka suluhu bila kufungana, lakini matokeo kama hayo yalipatikana zilipocheza mechi ya mzunguko wa pili Aprili 30, mwaka huu.

Fei Toto alifunga bao hilo kutokana na shambulizi hafifu langoni mwake, mabeki wa timu hiyo, wakauondoa, mpira ukamkuta mfungaji huyo ambaye aliukokota kwa umbali mrefu, huku wachezaji wa Simba badala ya kumfuata wakawa wanarudi nyuma na kuachia nafasi ya kulitazama goli, akiwa huru zaidi, kabla ya kuachia mkwaju mkwali wa juu, ulioshiba, ukaenda moja kwa moja upande wa kushoto kwa kipa Beno Kakolanya.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa inamsubiri mshindi wa mechi ya leo kati ya Azam dhidi ya Coastal Union utakapigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Iliichukua Yanga dakika tisa tu kubisha hodi kwenye lango la Simba, baada ya straika wake hatari, Fiston Mayele kumuacha Joash Onyango na kupiga shuti kali lililompita kipa Kakolanya, lakini mpira ukatoka sentimita chache kwenye lango.

Mayele tena, alimzidi nguvu Onyango, kiasi cha beki hiyo kuanguka chini, akapiga krosi fupi kwa Fei Toto ambaye aliachia kombora kali lililotoka nje kidogo ya lango dakika ya 16 ya mchezo, kabla ya kusawazisha makosa yake, dakika tisa baadaye.

Hadi inafungwa bao, Simba ilikuwa haijafanya shambulio lolote la maana langoni mwa wapinzani wao, hadi dakika ya 35 ilipopata faulo kutokana na Dennis Kibu kufanyiwa madhambi.

Hata hivyo, mpira wa faulo uliopigwa na Mohamed Hussein ulishindwa kutumiwa vizuri na Onyango ambaye alipiga kichwa nje kidogo ya lango.

Shambulizi la hatari zaidi kwa Simba kipindi cha kwanza lilikuwa dakika ya 37, Chris Mugalu alipounganisha kwa kichwa mpira wa faulo ya Tshabalala, lakini kipa wa Yanga, Djigui Diarra alijinyoosha upande wake wa kushoto na kwenda kudaka mpira huo.

Dakika moja baadaye, Mayele aliikosesha Yanga bao alipomuacha Onyango na kuingia hadi hatua tatu tu kutoka golini, lakini alikuwa mchoyo kwa kutaka kufunga mwenyewe, shuti lake hafifu likambabatiza Kakolanya na kuzagaa eneo la hatari, kabla hajauwahi na kuudaka.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko kadhaa kwa nyakati tofauti, Simba ikiwatoa Thadeo Lwanga aliyeumia, Mzamiru Yassin, Jimson Mwanuke na Kibu, wakiingia Rally Bwalya, Meddie Kagere, Yusuph Mhilu na Erasto Nyoni. Yanga ikiwatoa mfungaji wa bao, Fei Toto, Heritier Makambo, Kibwana Shomari na kuwaingiza Zawadi Mauya, Farid Mussa na Crispin Ngushi.

Kibwana na Kibu walitoka kutokana na kugongana kipindi cha pili ilipotokea heka heka langoni mwa Yanga, beki wa huo wa Yanga akitoka hapo hapo, wa Simba akitoka baadaye akiwa na jeraha kichwani akitoka baadaye.

Angalau kipindi cha pili, Simba ilifanya mashambulizi kadhaa langoni mwa Yanga, lakini hayakuwa na macho, nusura isawazishe dakika ya 90, baada ya kona iliyopigwa kichwa na Onyango, mpira ukagonga mwamba wa juu na kurejea uwanjani, ukamkuta Mhilu ambaye aliurudisha golini, lakini ukawababatiza mabeki wa Yanga na kurejea uwanjani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >